JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

**Unapojibu tafadhali taja:**

**Kumb. Na:**WDC/C.50/4/140 **Tarehe: 22 Oktoba, 2021**

Mhe. Mwenyekiti,
Mhe. Makamu Mwenyekiti na
Wah. Madiwani wote,
**Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.**

**YAH: MWALIKO WA KUHUDHURIA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI**

Tafadhali rejea somo la hapo juu.

Pamoja na barua hii, ninaomba kukualika kuhudhuria mkutano wa Kawaida wa Baraza la Madiwani uliopangwa kufanyika tarehe **28-29/10/2021** siku ya Alhamisi na Ijumaa. Muda wa kuanza mkutano ni saa **4:00** asubuhi, katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri.

Ajenda za mkutano pamoja na kablasha zimeambatishwa na barua hii.

Ninawatakia maandalizi mema.

*Maryam A. Muhaji*
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**WANGING'OMBE**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
WANGING'OMBE

***Nakala:*** Wakuu wa Idara/Vitengo Halmashauri ya Wilaya - kwa mahudhurio.
" Maafisa Tarafa Wilaya ya Wanging'ombe - kwa mahudhurio

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

**AJENDA ZA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 28-29.10.2021**

**1. AJENDA ZA TAREHE 28.10.2021**

1. Kufungua mkutano.
2. Kupokea ajenda za mkutano.
3. Kuapishwa Mhe. Diwani Kata ya Luduga.
4. Taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2021 Robo ya Kwanza kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, kutoka kwenye Kata ishirini na moja (21). Kata hizo ni:-
   - i. Ulembwe,
   - ii. Imalinyi,
   - iii. Mdandu,
   - iv. Wangama.
   - v. Udonja,
   - vi. Igosi,
   - vii. Kijombe,
   - viii. Itulahumba.
   - ix. Usuka,
   - x. Igwachanya,
   - xi. Uhenga,
   - xii. Luduga,
   - xiii. Igima,
   - xiv. Makoga.
   - xv. Saja
   - xvi. Kipengere
   - xvii. Malangali,
   - xviii. Ilembula,
   - xix. Wanging'ombe,
   - xx. Kidugala na
   - xxi. Uhambule,

**2. AJENDA ZA TAREHE 29.10.2021**

5. Salamu za Serikali Kuu.
6. Salamu za Chama Tawala (Chama cha Mapinduzi).
7. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa tarehe 05-06/08/2021.
8. Kusoma na kujadili utekelezaji wa maazimio ya mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa tarehe 05-06/08/2021.
9. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa mkutano maalum wa Baraza la Madiwani wa tarehe 23.09.2021.
10. Taarifa za Kamati za Kudumu za Halmashauri. Kamati hizo ni:-
    - i. Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango,
    - ii. Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi, Maliasili na Mazingira na
    - iii. Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji),
11. Taarifa mbalimbali:-

i. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2021 Robo ya Kwanza 2021/2022.
ii. Taarifa ya Soko la Igagala.

12. Taarifa za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kutoka Sekta zingine za Serikali ndani ya Halmashauri, zilizoalikwa kuwasilisha taarifa zake kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani, Sekta hizo ni pamoja na:-
    i. TANESCO.
    ii. WANGIWASA.
    iii. TARURA.
    iv. RUWASA.
13. Taarifa ya Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri.

14. Masuala ya Kiutumishi.

15. Kufunga mkutano.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**

# MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 05-06/08/2021 SIKU YA ALHAMISI NA IJUMAA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 05-06/08/2021 SIKU YA ALHAMISI NA IJUMAA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Agnetha J. Mpangile | Diwani Kata ya Ulembwe – Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya – **Mwenyekiti** |
| 2 | Ndg. Ferd Y. Mhanze | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji - **Katibu** |
| 3 | Mhe. Onesmo J. Lyandala | Diwani Kata ya Imalinyi – Makamu Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya - **Mjumbe** |
| 4 | Mhe. Fredrick E. Mwalongo | Diwani Kata ya Wangama - Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi na Mazingira- **Mjumbe** |
| 5 | Mhe. Anaupendo E. Gombela | Diwani Kata ya Mdandu – Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji) - **Mjumbe** |
| 6 | Mhe. Happiness B. Bomber | Diwani Kata ya Udonja – Mwenyekiti Kamati ya Maadili ya Madiwani - **Mjumbe** |
| 7 | Mhe. Oliver H. Myale | Diwani Kata ya Ilembula - **Mjumbe** |
| 8 | Mhe. Yustin L. Gudaga | Diwani Kata ya Usuka - **Mjumbe** |
| 9 | Mhe. Wiston E. Mbilinyi | Diwani Kata ya Kidugala – **Mjumbe** |
| 10 | Mhe. Damasco E. Mgaya | Diwani Kata ya Igosi – **Mjumbe** |
| 11 | Mhe. Anna D. Madembwe | Diwani Viti maalumu Tarafa ya Imalinyi – **Mjumbe** |
| 12 | Mhe. Jane F. Kisakanike | Diwani Viti maalum Tarafa ya Wanging'ombe – **Mjumbe** |
| 13 | Mhe. Joseph R. Mjujulu | Diwani Kata ya Uhambule – **Mjumbe** |
| 14 | Mhe. Andrew G. Mangula | Diwani Kata ya Saja – **Mjumbe** |
| 15 | Mhe. Geofrey K. Nyagawa | Diwani Kata ya Wanging'ombe – **Mjumbe** |
| 16 | Mhe. Anthon E. Mahwata | Diwani Kata ya Igwachanya– **Mjumbe** |
| 17 | Mhe. Mussa A. Sanga | Diwani Kata ya Kipengere – **Mjumbe** |
| 18 | Mhe. Thobias M. Mkane | Diwani Kata ya Itulahumba - **Mjumbe** |
| 19 | Mhe. Silvester J. Kigola | Diwani Kata ya Kijombe – **Mjumbe** |
| 20 | Mhe. Paulina S. Mwinami | Diwani Kata ya Igima – **Mjumbe** |
| 21 | Mhe. Halfan R. Kawambwa | Diwani Kata ya Uhenga – **Mjumbe** |
| 22 | Mhe. Magreth A. Kaduma | Diwani Viti maalum Tarafa ya Mdandu – **Mjumbe** |
| 23 | Mhe. Essau Th. Sanga | Diwani Kata ya Malangali – **Mjumbe** |
| 24 | Mhe. Victoria B. Mbiduka | Diwani Viti maalum Tarafa ya Imalinyi – **Mjumbe** |
| 25 | Mhe. Jelitha A. Fute | Diwani Viti maalum Tarafa ya Wanging'ombe – **Mjumbe** |
| 26 | Mhe. Jairos L. Lunyungu | Diwani Kata ya Makoga - **Mjumbe** |
| 27 | Mhe. Vumilia E. Kilamlya | Diwani Viti maalum Tarafa ya Mdandu – |
| 28 | Mhe. Esteria E. Mbwilo | Diwani Viti maalum Tarafa ya Imalinyi – **Mjumbe** |

**WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA KWA TAARIFA**

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Dkt. Festo J. Dugange | Naibu Waziri wa Nchi OR- TAMISEMI na Mbunge Jimbo la Wanging'ombe - **Mjumbe** |

**WAKUU WA IDARA/VITENGO WALIOHUDHURIA TAREHE 05-06/08/2021**

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Odetha Banige | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |
| 2 | Ndg. Yusta A. Mwambembe | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 3 | Ndg. Joyce A. Mdemwa | Mratibu wa TASAF |
| 4 | Ndg. Frank E. Ngogo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira |
| 5 | Ndg. Ismail Lugemalila | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mkaguzi wa Ndani |
| 6 | Ndg. Mathias Lyabonga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 7 | Ndg. Halid Idd Issa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi |
| 8 | Ndg. Severine M. Mfuse | Kny Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki |
| 9 | Ndg. Omath Sanga | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 10 | Ndg. Mohamed Ilunga | Kny Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 11 | Mhandisi Samson Mloge | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 12 | Ndg. Carystus Kihaka | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 13 | Ndg. Rosemary Kapoma | Mratibu wa Mapambano Dhidi ya UKIMWI |
| 14 | Ndg. Felishan M. Shantiwa | Kny Afisa Ushirika |
| 15 | Ndg. Shimwe Manwingi | Kny Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 16 | Ndg. Juma Chalamila | Kny Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 17 | Ndg. Monica Mbanga | Afisa Usafirishaji |
| 18 | Ndg. Bernadeta C. Fivawo | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika |
| 19 | Ndg. Rukia Mwelelwa | Katibu TSC |
| 20 | Ndg. Naili S. Mbyopyo | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 21 | Ndg. Demetrio Mgeni | Mthibiti Ubora wa Shule |
| 22 | Ndg. Keneth A. Mgina | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 23 | Ndg. Mulokozi A. Kishenyi | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 24 | Dkt. Frank Chiduo | Mganga Mkuu Halmashauri ya Wilaya |
| 25 | Ndg. Bujah Cosmas | Afisa Ardhi |
| 26 | Ndg. Telephory Myamba | Afisa Biashara |

**MAAFISA TARAFA WALIOHUDHURIA TAREHE 05-06/08/2021**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Emanuel I. Kingu | Afisa Tarafa – Tarafa ya Mdandu |
| 2 | Ndg. Hamza I. Zacharia | Afisa Tarafa – Tarafa ya Imalinyi |
| 3 | Ndg. Damas Kavindi | Afisa Tarafa -Tarafa ya Wanging'ombe |

**WATENDAJI WA KATA WALIOHUDHURIA TAREHE 05/08/2021**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Beatrice S. Kiwone | Mtendaji Kata ya Igima |
| 2 | Ndg. Fransiska Haule | Mtendaji Kata ya Itulahumba |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Ndg. Yohana B. Haule | Mtendaji Kata ya Igwachanya |
| 4 | Ndg. Harid Kapela | Mtendaji Kata ya Ilembula |
| 5 | Ndg. Beth E. Mangula | Mtendaji Kata ya Wanging'ombe |
| 6 | Ndg. Shukran F. Njamasi | Mtendaji Kata ya Udonja |
| 7 | Ndg. Tuombe Kiduge | Mtendaji Kata ya Luduga |
| 8 | Ndg. Festo B. Mbakilwa | Mtendaji Kata ya Malangali |
| 9 | Ndg. Yasinta G. Lupumbwe | Mtendaji Kata ya Uhambule |
| 10 | Ndg. Adam M. Dononda | Mtendaji Kata ya Uhenga |
| 11 | Ndg. Babulege Gowele | Mtendaji Kata ya Usuka |
| 12 | Ndg. Exavery W. Vegula | Mtendaji Kata ya Saja |
| 13 | Ndg. Upendo A. Fute | Mtendaji Kata ya Wangama |
| 14 | Ndg. Tijara Kupaza | Mtendaji Kata ya Ulembwe |
| 15 | Ndg. Bathromeo S. Mgaya | Mtendaji Kata ya Igosi |
| 16 | Ndg. Hongera Myamba | Mtendaji Kata ya Mdandu |
| 17 | Ndg. Yovita M. Sanga | Mtendaji Kata ya Imalinyi |
| 18 | Ndg. Tulakela E. Msagala | Kny Mtendaji Kata ya Makoga |
| 19 | Ndg. Anyes Y. Chongolo | Mtendaji Kata ya Kijombe |
| 20 | Ndg. Agatha Mwakifuna | Mtendaji Kata ya Kipengere |
| 21 | Ndg. Boston Vahaye | Mtendaji Kata ya Kidugala |

**WAALIKWA WALIOHUDHURIA TAREHE 06/08/2021**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Lauteri J. Kanoni | Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe |
| 2 | Ndg. Edward N. Manga | Katibu Tawala Wilaya ya Wanging'ombe |
| 3 | Capt. G G Kimaro | Mshauri wa Jeshi la Akiba Wilaya ya Wanging'ombe |
| 4 | SSP. Magnus C. Milinga | Mkuu wa Polisi Wilaya ya Wanging'ombe |
| 5 | Ndg. Scholastica Assey | Mkuu TAKUKURU Wilaya ya Wanging'ombe |
| 6 | Ndg. Dennis J. Nyambea | Afisa Uhamiaji |
| 7 | Ndg. Frank Duwe | TAKUKURU |
| 8 | Mhandisi Anesporo Mwijuka | Kny Meneja TARURA |
| 9 | Mhandisi Stephen Haule | TARURA |
| 10 | Mhe. J.E. Muhoni | Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Wanging'ombe |
| 11 | Mhandisi Charles Mengo | Meneja RUWASA |
| 12 | Mhandisi Wilfred M. Gichogo | TM- WANGIWASA |

**WAANDISHI WA HABARI WALIOSHIRIKI TAREHE 06/08/2021**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Michael Kanna | Mwandishi wa Habari |

**SEKRETARIETI**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Peter E. Chaula | Mwandishi wa Vikao |
| 2 | Ndg. Huruma O. Panja | Mwandishi wa Vikao |

**AJENDA ZA MKUTANO**

1. Kufungua mkutano.
2. Kupokea ajenda za mkutano.
3. Mheshimiwa Diwani Viti maalum Tarafa ya Mdandu kula Kiapo.
4. Taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021 Robo ya Nne kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, kutoka kwenye Kata ishirini na moja (21). Kata hizo ni:-
    i. Ulembwe,
    ii. Imalinyi,
    iii. Mdandu,
    iv. Wangama.
    v. Udonja,
    vi. Luduga,
    vii. Igima,
    viii. Makoga.
    ix. Igosi,
    x. Saja
    xi. Kijombe,
    xii. Usuka,
    xiii. Kipengere
    xiv. Malangali,
    xv. Uhenga,
    xvi. Igwachanya,
    xvii. Ilembula,
    xviii. Wanging'ombe,
    xix. Uhambule,
    xx. Kidugala na
    xxi. Itulahumba.

5. Salamu za Serikali Kuu.
6. Salamu za Chama Tawala/Chama cha Mapinduzi.
7. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa tarehe 29-30.04.2021.
8. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa mkutano maalum wa Baraza la Madiwani wa tarehe 07.06.2021.
9. Taarifa za Kamati za Kudumu za Halmashauri. Kamati hizo ni:-
    i. Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango,
    ii. Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi, Maliasili na Mazingira na
    iii. Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji),
10. Taarifa na mapendekezo mbalimbali:-
    i. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021 Robo ya Nne 2020/2021.
    ii. Mrejesho wa Bajeti ya Halmashauri kwa shughuli za maendeleo na matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
    iii. Rasimu ya Sheria Ndogo ya Uanzishaji wa Mfuko wa Elimu 2021 katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.
    iv. Mapendekezo ya Ratiba ya Vikao vya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

11. Taarifa za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kutoka Sekta zingine za Serikali ndani ya Halmashauri, zilizoalikwa kuwasilisha taarifa zake kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani, Sekta hizo ni pamoja na:-
    i. TARURA.
    ii. RUWASA.
    iii. WANGIWASA.
    iv. TANESCO.
12. Masuala ya Kiutumishi.
13. Kufunga mkutano.

**MUHTASARI NA. WDC/MBM/01/08/2021/2022 – KUFUNGUA MKUTANO**

1:1 Katibu alimtaarifu Mwenyekiti kuwa, mkutano huo ni wa kawaida kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji kwa kipindi cha kuishia mwezi Juni, 2021 robo ya nne (IV) kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

1:2 Ilielezwa kwamba, mkutano huo utafanyika kwa siku mbili, ambapo siku ya kwanza itatekelezwa ajenda ya Mheshimiwa Magreth Abisai Kaduma - Diwani Viti maalum Tarafa ya Mdandu kula kiapo pamoja na kupokea taarifa za Kata za utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa kipindi cha kuishia mwezi Juni, 2021, na siku ya pili ya tarehe 06.08.2021 zitapokelewa taarifa za utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo zilizotekelezwa na Menejimenti pamoja na Kamati za Kudumu kwa kipindi husika.

1:3 Baada ya hapo, alimjulisha Mwenyekiti kwamba, akidi ya wajumbe inaruhusu afungue mkutano.

1:4 Mwenyekiti alimkaribisha Makamu Mwenyekiti asome dua kwa ajili ya ufunguzi wa mkutano.

1:5 Kabla ya dua kusomwa Makamu Mwenyekiti aliwaomba wajumbe waimbe wimbo wa Taifa kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Halmashauri zinavyoongoza. Baada ya wimbo huo, Makamu Mwenyekiti alisoma dua.

1:6 Mwenyekiti aliwasalimu wajumbe, wataalam, waalikwa na watendaji wa kata na kuwakaribisha kwenye mkutano.

1:7 Mwenyekiti alimpa nafasi ya kuaga Bw. Emmanuel R. Kilundo aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji, baada ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI kumteua kuwa Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Mbeya, ambapo Bw. Emmanuel R. Kilundo aliwashukuru Viongozi kwa kumwogoza vizuri kwa kipindi chote alichotumikia Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.

1:8 Mwenyekiti alimtakia mafanikio mema Bw. Emmanuel R. Kilundo katika utendaji wa kazi kwa nafasi hiyo mpya ya kazi, pia alimshauri kwamba, aongeze ufanisi zaidi katika uwajibikaji ili kuendelea kujipatia sifa njema.

1:9 Baada ya hapo, Mwenyekiti alisoma hotuba ya ufunguzi wa mkutano.

1:10 Akisoma hotuba ya ufunguzi wa mkutano huo, **aliwaeleza** wajumbe mafanikio mbalimbali ya Halmashauri, yaliyopatikana kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021. Mafanikio hayo yalihusisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na utekelezaji wa shughuli za maendeleo Kisekta.

1:11 **Kuhusu ukusanyaji wa mapato,** ilielezwa kwamba, kuishia mwezi Juni, 2021 Halmashauri imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 2.92 sawa na asilimia 124.31 ya makisio ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

1:12 **Kuhusu utoaji wa mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu,** ilifahamishwa kwa wajumbe kwamba, kuishia mwezi Juni, 2021 Halmashauri imetoa mikopo inayogharimu shilingi Milioni 230.6 Wanawake vikundi 27 shilingi Milioni 169.9, Vijana shilingi Milioni 56.9, kwa vikundi 08 na watu Wenye Ulemavu shilingi Milioni 3.8 kwa vikundi 2.

1:13 **Kuhusu ukaguzi uliofanywa na Mkaguzi wa Nje (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/2020,** ilifahamishwa kwa wajumbe kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe imepata Hati Safi. Aidha, aliwakumbusha wajumbe kuwa, Halmashauri imeendelea kupata Hati Safi mfululizo kwa kipindi cha miaka saba, tangu ilipofanyiwa ukaguzi wa awali mwaka wa fedha 2013/2014.

1:14 Alipongeza ushirikiano uliopo kati ya Waheshimiwa Madiwani na Menejimenti ya Halmashauri kwa usimamizi mzuri wa rasirimali na shughuli mbalimbali za maendeleo ya Halmashauri zinazopelekea Halmashauri kuendelea kupata Hati safi katika kaguzi zote zilizofanyika.

1:15 Alisisitiza suala la Viongozi wa Vijiji kuhakikisha wanaweka mkazo katika kusoma mapato na matumizi ya vijiji kwa wananchi kwa mujibu wa miongozo iliyopo, ili kuweka uwazi wa michango wanayotoa wananchi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

1:16 Baada ya hotuba hiyo, Mwenyekiti alifungua mkutano saa **04:11** asubuhi.

**MUHTASARI NA. WDC/MBM/02/08/2021/2022 – KUPOKEA AJENDA**

2:1 **Katibu** alisoma ajenda kumi na tatu zilizoandaliwa na kuwasilisha kwa wajumbe.

2:2 Wajumbe walipokea na kuridhia ajenda zote kumi na tatu, kuwa zijadiliwe kwenye mkutano huo.

**MUHTASARI NA. WDC/MBM/03/08/2021/2022 – MHESHIMIWA DIWANI VITI MAALUM TARAFA YA MDANDU KULA KIAPO**

3:1 Mheshimiwa Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Wanging'ombe alimwongoza Mheshimiwa Magreth Abisai Kaduma kula kiapo cha uongozi, ambapo Mheshimiwa Diwani alikula kiapo cha uongozi kwa Imani yake ya Kikristo.

3:2 Baada ya kiapo hicho, Mkurugenzi Mtendaji alimkabidhi Vitendea kazi Mheshimiwa Magreth Abisai Kaduma Diwani Viti maalum Tarafa ya

Mdandu, ikiwa ni pamoja na joho la kuvaa kwenye mikutano ya Baraza la Madiwani.

3:3 Mwenyekiti alimkaribisha Mheshimiwa Magreth Abisai Kaduma katika umoja wa Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.

3:4 Alimpa nafasi Mheshimiwa Magreth Abisai Kaduma aseme neno la shukrani kwa wajumbe.

3:5 Mheshimiwa Magreth Abisai Kaduma aliwashukuru wajumbe kumpokea na kuwapa pole Waheshimiwa Madiwani kwa kuondokewa na Mheshimiwa Mwamini J. Wikesi aliyekuwa Diwani Viti maalum Tarafa ya Mdandu na Mheshimiwa Hassan T. Ngella aliyekuwa Diwani Kata ya Luduga.

**MUHTASARI NA. WDC/MBM/04/08/2020/2021 – TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI APRILI HADI JUNI, 2021 ROBO YA NNE KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021, KUTOKA KWENYE KATA ISHIRINI NA MOJA (21)**

4:1 Kabla ya kuwasilishwa taarifa hizo kwa utaratibu wa kila Diwani wa Kata husika kuwasilisha taarifa yake, Makamu Mwenyekiti aliwasilisha ombi kwa Mwenyekiti kuwa, kutokana na kuwepo kwa wimbi la tatu la UVIKO 19 inaombwa taarifa za kata zote 21 ziwasilishwe kwa ujumla wake.

4:2 Ilishauriwa kwamba, Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Wataalam wake wapitie kwa kina taarifa hizo kupitia vikao vya Menejimenti ili kuainisha changamoto zilizopo kwenye kila Kata.

4:3 Ilielezwa kwamba, baada ya kutambua changamoto za kila Kata, Menejimenti itafute ufumbuzi wa kila changamoto na kufanya utekelezaji wake. Mrejesho wa ufumbuzi/utekelezaji wa kila changamoto uwasilishwe kwenye kila Kata.

4:4 Ombi hili pamoja na ufafanuzi wake ulipokelewa na wajumbe na kupitishwa bila hoja.

4:5 Ilitaarifiwa kwa wajumbe kwamba, Menejimenti itazipitia taarifa hizo na kuzifanyia kazi, na kutoa mrejesho wa utekelezaji wake kwa kila Kata.

4:6 **AZIMIO:** Mrejesho wa ufumbuzi/utatuzi wa changamoto za kila Kata zilizoainishwa kwenye taarifa zilizowasilishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe 5.08.2021 uwasilishwe kwenye Kata zote 21 kwa barua (Watendaji wa Kata zote wafahamishwe kwa barua).

4:7 Wajumbe waliridhia na kupitisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021 robo ya nne kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kutoka kwenye kata ishirini na moja ili ziwe kumbukumbu za kudumu za Halmashauri.

4:8 **Kuahirisha mkutano tarehe 05.08.2021**

4:8:1 Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki mkutano huo na kufanikisha kutekeleza shughuli zilizopangwa kufanyika tarehe hiyo.

4:8:2 Mwenyekiti aliahirisha mkutano saa **04:49** asubuhi siku ya Alhamisi ya tarehe **05.08.2021.**

4:9 **Mwendelezo wa mkutano tarehe 06.08.2021**

4:9:1 Mkutano ulianza saa **04:21** asubuhi.

4:9:2 Kabla ya kuendelea na ajenda za mkutano kwa tarehe hiyo, Katibu alifanya utambulisho wa uwepo wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya, RUWASA, TARURA na WANGIWASA (wajumbe waalikwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani).

**MUHTASARI NA. WDC/MBM/05/08/2021/2022 – SALAMU ZA SERIKALI KUU**

5:1 Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe aliwasilisha salamu za Serikali Kuu kwa wajumbe wa mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe 06.08.2021.

5:2 Akiwasilisha salamu hizo, alianza kwa kuwasalimu wajumbe na kuwapa pole wajumbe kwa kuondokewa na Mheshimiwa Hassan Talangimbudza Ngella aliyekuwa Diwani Kata ya Luduga.

5:3 Alipongeza Baraza la Madiwani kwa uendeshaji mzuri wa Halmashauri na uongozi mzuri unaojionesha katika ufanisi wa masuala mbalimbali ikiwemo matumizi sahihi ya fedha za Serikali.

5:4 Vile vile aliipongeza Halmashauri kwa kuendelea kung'ara kwa kupata Hati Safi za ukaguzi wa nje unaofanywa na CAG kwa miaka saba mfululizo, tangu Halmashauri ilipoanzishwa mwaka 2013.

5:5 **Kuhusu ulinzi na usalama,** ilielezwa kwamba, elimu iendelee kutolewa kwa wananchi kutojichukulia sheria mkononi, badala yake mambo yaweyanaendeshwa kisheria kwa kutumia vyombo vilivyowekwa na Serkali. Ilishauriwa viongozi kuwahamasisha vijana kujiunga na mafunzo ya Jeshi la akiba ili kuimarisha ulinzi shirikishi ngazi ya jamii.

5:6 **Kuhusu mbio za Mwenge Maalum wa Uhuru 2021,** ilishauriwa kwamba, viongozi waendelee kusimamia vyema miradi ya Mwenge inayotekelezwa katika maeneo yao, ili ikamilike kwa wakati, wananchi wahamasishwe kujitokeza kwa maeneo yote ambayo Mwenge utapita.

5:7 **Kuhusu tahadhari ya UVIKO - 19,** ilishauriwa kwamba, viongozi wawahamasishe wananchi kuendelea kuchua tahadhali kwa kunawa mikono na maji tiririka kwa sabuni, kuvaa barakoa, kutochangia chombo kimoja, hasa wakati wa kunywa pombe na kuepuka misongamano. Wananchi, waelekezwe kijitokeza kwa hiari kufika kwenye vituo vya Afya vilivyokaribu yao ili kupata chanjo ya UVIKO – 19.

5:8 **Kuhusu ukamilishaji wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya mapokezi ya kidato cha kwanza 2022,** iliagizwa kwamba, kasi iongezwe ya ujenzi

madarasa yanayoendelea kujengwa katika shule mbalimbali za sekondari ili yakamilike kwa wakati bila kuathiri viwango vya ubora unaotakiwa. Kwa Kata ambazo hazina shule zitumie muda uliobako kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa vinavyohitajika na vitu vingine muhimu, ili shule za Kata husika zipate usajili kabla ya mwezi Januari, 2022.

5:9 Ilisisitizwa kwamba, kwa mwaka 2022 hapatakuwa na mtoto atakayepangiwa shule ya sekondari nje ya kata yake.

5:10 **Kuhusu usimamizi wa miradi,** ilishauriwa viongozi wawe wanatembelea miradi inayotekelezwa katika maeneo yao kila mara, na wanapobaini mapungufu taarifa ziwe zinatolewa kwa Mkurugenzi Mtendaji kwa wakati, ili marekebisho yawe yanafanyika kwenye hatua za awali, kutokana na kutokea kwa malalamiko kwa baadhi ya maeneo kulazimika kubomoa tofali.

5:10:1 Ilielezwa kwamba, miradi mingi inayotekelezwa inachangamoto ya kupokea tofali zilizo chini ya kiwango kutoka kwa wazabuni, baada ya hapo iliagizwa kwamba, wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe walio na uwezo wa kutoa huduma za zabuni mbalimbali ikiwemo kuuza tofali wajengewe uwezo ili waanze kutoa huduma kwa Halmashauri, ili waweze kunufaika na fedha ya Serikali inayoletwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.

5:11 **Kuhusu i-CHF iliyoboreshwa,** ilishauriwa viongozi wawahamasishe wananchi kujiunga na i-CHF ili wawe na uhakika wa kupata matibabu.

5:12 **Kuhusu mapato ya Halmashauri,** aliipongeza Halmashauri kwa kukusanya mapato na kuvuka lengo kwa mwaka 2020/2021 kwa kufikisha asilimia 176. Ambapo, ilipangwa kukusanywa TZS. 1,660,266,000/= na imekusanya jumla ya TZS. 2,921,359,669/=.

5:12:1 Vile vile ilishauriwa kwamba, viongozi na wataalam waendelee kufanya kazi kwa ushirikiano ili kufikia lengo la ukusanyaji mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2021/2022 la jumla ya TZS. 2,400,000,000/=.

5:12:2 Ilishauriwa kwamba, fedha zinazopatikana zitumike vizuri katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Wanging'ombe.

5:13 **Kuhusu vita dhidi ya udumavu,** ilishauriwa kwamba, katika mikutano yote inayofanywa na viongozi ngazi ya vijiji/kata ajenda ya kutoa elimu ya lishe iwe ni ya kudumu,

5:13:1 Ilielezwa kwamba, wananchi waelimishwe suala la lishe kwa kuzingatia mpango shuruti wa Wilaya ulioandaliwa kupitia sheria ndogo za vijiji ili kuwabaini wanaokiuka maelezo ya wataalam na kusababisha udumavu.

5:14:1 Ilisisitizwa kwamba, viongozi waupokee mpango huo na kuusimamia ili Wilaya ya Wanging'ombe uondokane na udumavu.

5:15:2 **Iliagizwa** kwamba, ajenda ya lishe iwe ni ya kudumu kwenye vikao vya KAMAKA na Kamati za Kudumu za Halmashauri.

5:16 Ilishauriwa Waheshimiwa Madiwani wampokee Mkurugenzi aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais na kupangiwa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe na wampe ushirikiano ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuwaletea maendeleo wananchi.

5:16:1 Alimpongeza Mkurugenzi aliyekuwepo kwa kuwa msikivu, mbunifu na kufuata maelekezo ya viongozi ambayo yalimsaidia kufikia malengo ya Halmashauri katika kuwahudumia vizuri wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe.

5:17 Katika kuhitimisha uwasilishaji wa salamu za Serikali Kuu, Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, alisisitizwa kwamba, viongozi na watendaji waendelee kudumisha Mshikamano, Umoja na Upendo.

5:18 Mwenyekiti alimshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kuwasilisha salamu za Serikali Kuu.

5:18:1 Alimhakikishia kuwa, maagizo yote ya Serikali Kuu yamepokelewa na Halmashauri itayafanyia kazi ipasavyo.

**MUHTASARI NA. WDC/MBM/06/08/2021/2022 – SALAMU ZA CHAMA TAWALA (CHAMA CHA MAPINDUZI)**

6:1 Mhe. Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Wanging'ombe aliwasilisha salamu za Chama Tawala/Chama Cha Mapinduzi kwa wajumbe wa mkutano wa Baraza la Madiwani tarehe 06.08.2021.

6:2 Alianza kwa kuwasalimu wajumbe na kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuwajalia uzima, afya na kukutana katika mkutano huo.

6:3 Aliwapa pole wajumbe kwa kuondokewa na Mheshimiwa Hassan Talangimbudza Ngella, aliyekuwa Diwani Kata ya Luduga na kuiombea roho ya marihemu, Mungu aipumzishe kwa amani.

6:4 Alishukuru kupata nafasi ya kuwasilisha salamu za Chama Tawala kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani kwa mara ya kwanza tangu kuisha kwa uchaguzi na Baraza la Madiwani kuundwa 2020.

6:5 Aliwapongeza na kuwashukuru watendaji kwa kusimamia vizuri uchaguzi uliofanyika 2020 wa Rais, Wabunge na Madiwani.

6:6 Aliwapongeza Waheshimiwa Madiwani kwa kupata nafasi hiyo na kuwataka waendelee kuisimamia Halmashauri ili kuwaletea maendeleo wanawanging'ombe.

6:7 Aliwapongeza Waheshimiwa Madiwani na Watendaji kwa kazi nzuri ya ukusanyaji wa mapato ambapo Halmashauri imevuka lengo la ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Alisisitiza kuongeza jitihada ya ukusanyaji mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ili fedha itakayopatikana isaidie kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi.

6:8 Aliwakumbusha Waheshimiwa Madiwani kwamba, uwajibikaji wao wa kuwaletea wananchi maendeleo, utapimwa baada ya miaka mitano ijayo

na kuwashauri kwamba, waisimamie vizuri Halmashauri ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

6:9 Aliwashauri Waheshimiwa Madiwani kwamba, changamoto zote zinazojitokeza katika Halmashauri na katika nafasi zao wawe wanazimaliza kupitia vikao.

6:10 Alisisitiza kwamba, utekelezaji wa miradi ya maendeleo uzingatie viwango vya ubora unaotakiwa.

6:11 Kuhusu mikopo inayotolewa na Halmashauri kwa vikundi vya Vijana, ilishauriwa vijana wahamasishwe kuanzisha viwanda vya kutengeneza tofali ili Halmashauri iweze kununua tofali hizo kwa ajili ya ujenzi wa majengo mbalimbali ya Serikali.

6:12 Aliwaagiza Waheshimiwa Madiwani kuwahamasisha wananchi kufanya kazi katika maeneo yao ili kujiongezea kipato.

6:13 Kuhusu UVIKO - 19, ilishauriwa viongozi wawahamasishe wananchi kujitokeza kupata chanjo.

6:14 Akihitimisha uwasilishaji wa salamu za Chama Tawala/Chama Cha Mapinduzi kwa wajumbe wa mkutano wa Baraza la Madiwani, alimshukuru Mwenyekiti wa Halmashauri kumpa nafasi hiyo, alimpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri.

6:15 Mwenyekiti alishukuru kuwasilishwa kwa salamu za Chama Tawala/Chama cha Mapinduzi, kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani. Alimtakia majukumu mema Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Wanging'ombe katika kusimamia Chama.

**MUHTASARI NA. WDC/MBM/07/08/2021/2022 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 29-30.04.2021**

7:1 Muhtasari wa mukutano wa tarehe 29-30.04.2021 ulisomwa na kuwasilishwa kwa Wajumbe.

7:2 Wajumbe walipokea na kupitia muhtasari huo.

7:3 Wajumbe waliridhia yaliyojadiliwa katika mkutano huo na kupitisha kwamba, Mwenyekiti na Katibu wasaini muhtasari wa mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe 29-30.04.2021 ili iwe kumbukumbu sahihi ya shughuli za Halmashauri.

**MUHTASARI NA. WDC/MBM/08/08/2021/2022 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO MAALUM WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 07.06.2021**

8:1 Muhtasari wa mkutano maalum wa tarehe 07.06.2021 ulisomwa na kuwasilishwa kwa Wajumbe.

8:2 Wajumbe walipokea na kupitia muhtasari huo.

8:3 Wajumbe waliridhia yaliyojadiliwa katika mkutano huo maalum na kupitisha kwamba, Mwenyekiti na Katibu wasaini muhtasari wa mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe 07.06.2021 ili iwe kumbukumbu sahihi ya shughuli za Halmashauri.

**MUHTASARI NA. WDC/BM/09/08/2021/2022 – TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI, KWA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI APRILI HADI JUNI, 2021 ROBO YA NNE (IV) KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

9:1 **Taarifa ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango**

9:1:1 Taarifa ya shughuli ambazo Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango imezitekeleza kwa kipindi cha kuishia Juni, 2021 ilisomwa na kuwasilishwa kwa wajumbe.

9:1:2 Ilielezwa kwa wajumbe kwamba, shughuli ambazo Kamati imezitekeleza kwa kipindi hicho ni pamoja na kufanya vikao, kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kuidhinisha matumizi mbalimbali ya fedha, kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo na kufuatilia utekelezaji wa maazimio na maagizo ya vikao.

9:1:3 Wajumbe walipokea na kuipitia taarifa hiyo.

9:1:4 **Majadiliano**

9:1:4:1 Kuhusu azimio la Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwenda kujifunza kwenye Halmashauri zingine mbinu za ukusanyaji wa mapato, wajumbe walieleza kwamba, uwezo wa Halmashauri wa kukusanya mapato kwa sasa ni mkubwa, kwani, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imevuka lengo.

9:1:4:1:1 Ilishauriwa kwamba, kwa kuwa Halmashauri inauwezo mzuri wa kukusanya mapato unaotokana na usimamizi mzuri wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango, ni vema ziara ya Kamati kujifunza kwenye Halmashauri zingine isifanyike badala yake Halmahauri zingine zije kujifunza katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.

9:1:4:1:2 Ilifafanuliwa kwa wajumbe kwamba, lengo la Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kuazimia kwenda kujifunza katika Halmashauri zingine ni kupata mbinu zingine mpya zaidi za uibuaji wa vyanzo vya mapato, vile vile kujifunza mbinu za kuboresha vyanzo vya mapato vilivyopo ili kuongeza tija zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani.

9:1:4:1:3 Wajumbe walipokea ufafanuzi huo na kuridhia kwamba, Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango iendelee na utekelezaji wa azimio hilo.

9:1:4:2 Kuhusu posho za mwezi za Waheshimiwa Madiwani kulipwa na Serikali Kuu, wajumbe walieleza kwamba, Serkali imeipunguzia mzigo Halmashauri wa kulipa posho za mwezi kwa Waheshimiwa

Madiwani, kwa kuanza kuwalipwa posho hizo Waheshimiwa Madiwani.

9:1:4:2:1 Baada ya maelezo hayo, ilishauriwa kwamba, kutokana na Halmashauri kuwa na uwezo mzuri wa ukusanyaji mapato ya ndani, ni vema ikaonwa namna ya kuanza kuwalipa posho Wenyeviti wa Vijiji kiasi cha TZS. 50,000/=.kwa mwezi.

9:1:4:2:2 Vile vile ilipendekezwa kwamba, Waheshimiwa Madiwani waongezewe posho kupitia mapato ya ndani kiasi cha TZS. 150,000/= kwenye posho ya mwezi.

9:1:4:2:3 Ilifafanuliwa kwa wajumbe kwamba, Halmashauri pamoja na Serikali inatambua uwepo wa wenyeviti wa vijiji. Kuwalipa posho wenyeviti wa vijiji na kuongeza posho ya Madiwani ni jambo la muhimu, kinachotakiwa ni kufuata miongozo ya Serikali na uwepo wa bajeti ya Halmashauri ya kulipa posho hizo.

9:1:4:2:4 Ilielezwa kwamba, hakuna mwongozo wa Serikali unaoruhusu Halmashauri kutoa posho kwa wenyeviti wa vijiji.

9:1:4:2:5 Wajumbe walishauri kwamba, pamoja na kuzingatia miongozo ya Serikali, Halmashauri kupitia vikao vya Menejimenti na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ione uwezekano wa kuanza kutoa motisha kwa wenyeviti wa vijiji, ili kuwaongezea ari ya kusimamia maendeleo katika maeneo yao.

9:1:4:3 Wajumbe walipitisha na kuridhia taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa kipindi cha kuishia mwezi Juni, 2021, iwe kumbukumbu sahihi ya shughuli za Halmashauri.

9:2 **Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi, Maliasili na Mazingira**

9:2:1 Taarifa ya shughuli ambazo Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi, Maliasili na Mazingira imezitekeleza kwa kipindi husika ilisomwa na kuwasilishwa kwa wajumbe.

9:2:2 Ilielezwa kwa wajumbe kwamba, shughuli ambazo Kamati hii imezitekeleza kwa kipindi cha kuishia mwezi Juni, 2021 ni pamoja na kufanya vikao, kupitia na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa shughuli za maendeleo zilizowasilishwa kwenye vikao kutoka Sekta mbalimbali za Kiuchumi na kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya vikao.

9:2:3 Wajumbe waliipokea na kuipitia taarifa hiyo.

9:2:4 Wajumbe walipitisha na kuridhia taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kipindi cha kuishia mwezi Juni, 2021 iwe kumbukumbu sahihi ya shughuli za Halmashauri.

9:3 **Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji)**

9:3:1 Taarifa ya shughuli ambazo Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji) imezitekeleza kwa kipindi husika ilisomwa na kuwasilishwa kwa wajumbe.

9:3:2 **Ilitaarifiwa** kwa Wajumbe kwamba, shughuli ambazo Kamati hii, imezitekeleza kwa kipindi cha kuishia mwezi Juni, 2021 ni pamoja na: kufanya vikao, kupitia na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa shughuli za maendeleo zilizowasilishwa kwenye vikao kutoka Sekta mbalimbali za Kijamii (Elimu, Afya na Maji) na kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya vikao.

9:3:3 Wajumbe walipokea na kuipitia taarifa hiyo.

9:3:4 Wajumbe walipitisha na kuridhia taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji) kwa kipindi cha kuishia Juni, 2021 iwe kumbukumbu sahihi ya shughuli za Halmashauri.

**MUHTASARI NA. WDC/MBM/10/08/2021/2022 – TAARIFA MBALIMBALI:**

10:1 **Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021**, ilisomwa na kuwasilishwa kwa wajumbe.

10:1:1 Ilitaarifiwa kwa wajumbe kwamba, katika mwaka wa fedha 2020/21 kiasi cha Tshs. 8,290,885,111 kiliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Kiasi hicho kinajumuisha Shs. 4,320,636.172.00 fedha za ndani na Shs 3,078,554,000.00 fedha za nje. Kiasi cha Shs. 940,000,000.00 kiliidhinishwa ikiwa ni fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuchangia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

10:1:2 Katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2021, jumla ya Shs. 3,884,768,125.94 zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Maendeleo ikiwa ni sawa na 52.50% ya fedha iliyokisiwa. Fedha zilizopokelewa zinajumuisha mifuko ya TASAF, UNICEF, EP4R katika Idara ya Elimu, Mfuko wa pamoja wa Afya (HBF) na Fedha za Elimu Bure.

10:1:3 Ilielezwa kwamba, fedha hizi zinaendelea kutekeleza Miradi ya Maendeleo katika maeneo mbalimbali katika Halmashauri yetu kwa Bajeti ya Mwaka 2020/2021.

10:1:4 Ilifafanuliwa kwamba, katika taarifa hii, kuna utekelezaji wa Mradi Kiporo Mmoja wa Mwaka 2019/2020 ambao umeendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021. Mradi huu upo katika jedwali ukurasa wa 1.

10:1:5 Aidha, Halmashauri imepokea fedha kiasi cha Shs.2,079,200,000.00 ikiwa ni ongezeko la bajeti ya Mwaka 2020/2021 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Idara za Elimu na Afya.

10:1:6 Ilijulishwa kwa wajumbe kwamba, kwa ujumla hali ya utekelezaji wa Miradi katika Robo hii ya Nne ya mwaka 2020/21 umekuwa mzuri kwa kuwa Halmasahuri imepokea fedha kutoka Serikali Kuu kwa Mujibu wa Bajeti. Michanganuo ya Mapokezi ya fedha hizo imeoneshwa katika majedwali yaliyoambatishwa.

10:17 Aidha, Utekelezaji wa shughuli za Maendeleo katika kipindi cha Robo hii haukuwa na changamoto nyingi kwa kuwa Serikali Kuu (Wizara ya Fedha na Mipango) Imeendelea kuleta fedha kwa ajili ya kumalizia na kuanza Ujenzi wa Miradi Mikubwa na Midogo ndani ya Halmashauri. Michanganuo ya mapokezi ya fedha ipo katika ukurasa wa 2 wa taarifa.

10:1:8 Ilielezwa kwa wajumbe kwamba, Muhtasari huu umeambatana na majedwali ya ufafanuzi wa utekelezaji katika shughuli za maendeleo kwa kila Sekta na vyanzo vya fedha pamoja na hali halisi ya utekelezaji wa miradi mbalimbali. Majedwali haya ni kama yanavyoonekana kuanzia Ukurasa wa 3 – 20 katika taarifa hiyo.

10:1:9 Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuipitia ukurasa kwa ukurasa.

10:1:10 **Majadiliano**

10:1:10:1 Kuhusu Serikali kuleta fedha za miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, wajumbe waliipongeza Serikali Kuu kwa kuleta fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri.

10:1:10:2 Kuhusu miradi inayotekelezwa kwa Force Account, iliwasilishwa taarifa kwamba, baadhi ya Kata viongozi hawashirikishwi kikamilifu katika kutoa ushauri unaotakiwa kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo, badala yake ujenzi wa miradi huanza bila ya viongozi wa eneo husika kufahamu, matokeo vyoo vinajengwa karibu na madarasa mfano Shule ya Msingi Mng'erenge choo kimejengwa karibu na darasa.

10:1:10:2:1 Ilishauriwa kwamba, Waheshimiwa Madiwani wawe wanashirikishwa kikamilifu, katika kupata maelekezo ya mwanzo, ambayo Kamati za Ujenzi wa miradi inayojengwa kwa Force account hupewa, kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi husika, ili kujenga uelewa wa pamoja kati ya Waheshimiwa Madiwani na Kamati za Ujenzi.

10:1:10:2:2 Vile vile ilishauriwa kwamba, mwongozo wa uundaji wa Kamati za Ujenzi wa miradi inayotekelezwa kwa Force Account, uangaliwe namna ya kuufanyia marekebisho ili watendaji wa maeneo husika wawe Wenyeviti wa Kamati badala ya Walimu Wakuu, ambao kwa mujimu wa mwongozo ni Wenyeviti wa Kamati za Manunuzi kwa miradi inayotekelezwa kwenye Shule za Msingi na Shule za Sekondari. Ilielezwa kwamba, kwa kuweka utaratibu huo itasaidia walimu kuendelea na shughuli ya kuu ya kufundisha na watendaji kusimamia miradi ya maendeleo.

10:1:10:2:3 Pia ilielezwa kwamba, Kamati za Ujenzi zinakabiliwa na changamoto ya kukosa fedha ya nauli ya kufuatilia vifaa vinavyotakiwa kununuliwa, kutokana na fedha za mradi zinazotolewa kukosa kipengele cha matumizi mengineyo, fedha yote ni kwa matumizi ya mradi tu.

10:1:10:2:4 Ilishauriwa kwamba, Menejimenti ione namna ya kuziwezesha Kamati za Ujenzi kupata fedha za ufuatiliaji wa vifaa vya ujenzi.

10:1:10:2:5 Ilifafanuliwa kwa wajumbe kwamba, ushirikishwaji upo wa kutosha, kwa jamii na viongozi wa eneo ambalo mradi unatekelezwa, ushirikishwaji huo huhusisha viongozi ngazi ya Kijiji na Kata husika.

10:1:10:2:6 Ilielezwa kwamba, mawasiliano yataimarishwa ili maeneo yote viongozi wawe wanashirikishwa kikamilifu kuanzia mwanzo hadi mwisho wa utekelezaji wa miradi inayotumia utaratibu wa Force Accounti katika utekelezaji wake.

10:1:10:2:7 Vile vile ilifafanuliwa kwamba, fedha zinazotolewa na Serikali Kuu, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi inayotakiwa kutumia Force Account zinatolewa pamoja na mwongozo wa namna ya utekelezaji na uundaji wa kamati za ujenzi na nani anatakiwa kuwa Mwenyekiti katika kila Kamati.

10:1:10:2:8 Ilishauriwa kwa wajumbe kwamba, ni muhimu kufuata na kuzingatia mwongozo katika utekelezaji wa miradi hiyo, ili kuepuka hoja za ukaguzi. Ilielezwa kwamba, kinachotakiwa ni kuimarisha usimamizi na mawasiliano kati ya Kamati za Ujenzi na Viongozi wa maeneo husika ili kushirikiana kwa pamoja katika usimamizi wa miradi hiyo.

10:1:10:2:9 Kuhusu kuziwezesha Kamati za Ujenzi kufuatilia vifaa vya ujenzi, iliombwa kwamba Kamati za Maendeleo ya Kata (KAMAKA) na Serikali za Vijiji ziwe zinasaidia Kamati za Ujenzi kupata nauli ya ufuatiliaji wa vifaa vya ujenzi.

10:1:10:2:10 Wajumbe walipokea ufafanuzi huo na kuagiza menejimenti izingatie yafuatayo:

i. Menejimenti ifuatilie kwa kina katika maeneo yote yenye miradi inayotekelezwa kwa kuunda Kamati za Ujenzi, ili kubaini mapungufu yanayolalamikiwa na viongozi.

ii. Barua ziwe zinaandikwa kwa wakati kwa Waheshimiwa Madiwani za kuwapa taarifa za ujio wa fedha katika Kata husika za miradi inayotekelezwa kwenye ngazi ya Kata na Kijiji.

iii. Wataalam wanapotembelea miradi katika ngazi ya Kata na Kijiji wawe wanawapa taarifa Waheshimiwa Madiwani wa eneo husika ili wawepo katika eneo la mradi kupokea maelekezo ya kitaalam kuhusu uboreshaji wa mradi husika.

iv. Wenyeviti wa Kamati za Ujenzi waelekezwe kusikiliza ushauri wa viongozi wa Kata/Waheshimiwa Madiwani wa eneo husika katika kuboresha utekelezaji wa miradi ya shule na afya. Pia waelekezwe kuwashirikisha viongozi wa maeneo husika.

v. Menejimenti itoe miongozo kwa Kamati za Ujenzi inayowapa nguvu viongozi wa Kata/Waheshimiwa Madiwani katika kusimamia miradi ya ujenzi, kutokana na viongozi kuonekana hawana nguvu katika kusimamia miradi hiyo.

10:1:10:2:10:1 Kuhusu Wataalam kupita katika maeneo mbalimbali kukagua miradi, ilifahamishwa kwa wajumbe kwamba, wataalam wa eneo husika hufahamishwa ujio wa Wataalam kutoka Ofisi ya Mkurugenzi katika maeneo yao. Wataalam hao wanapaswa kuwajulisha viongozi katika maeneo yao ujio wa Timu ya Wataalam kutoka Ofisi ya Mkurugenzi.

10:1:10:2:10:2 Kuhusu kuwajulisha Waheshimiwa Madiwani mapokezi ya fedha za miradi katika maeneo yao, ilielezwa kwamba, itazingatiwa na kutekelezwa.

10:1:10:3 Kuhusu Fedha za Kapu la Pamoja/Basket Fund, wajumbe walipitia matumizi ya fedha za Mfuko huo na kueleza kwamba, matumizi mengi ya fedha za Mfuko huo, zimeelekezwa katika kufanya Semina kwa watumishi, badala ya kuelekezwa kwenye shughuli za miradi ya maendeleo.

10:1:10:3:1 Baada ya maelezo hayo, iliulizwa ni kwa nini fedha hizo hazielekezwi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo?

10:1:10:3:2 Ilifahamishwa kwa wajumbe kwamba, fedha ya Kapu la Pamoja zinamwongozo wa matumizi yake na lengo la fedha hizo ni kuimarisha rasirimali watu katika utendaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo.

10:1:10:3:3 Ilitaarifiwa kwa wajumbe kwamba, kiasi cha fedha hizo hutumika katika kutekeleza miradi mfano kufanya ukarabati wa miundombinu ya majengo ya vituo vya kutolea huduma za afya.

10:1:10:3:4 Wajumbe walishauri kwamba, ushirikishwaji uwe unafanyika kwa viongozi, ili wawe wanajua maeneo ambayo fedha za Kapu la Pamoja zimetumika katika kufanya ukarabati wa majengo ya kutolea huduma za afya.

10:1:10:4 Kuhusu usimamizi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya shule, ilishauriwa kwamba, Mhandisi wa Ujenzi awe anakagua hatua moja na kuruhusu kuendelea na hatua nyingine katika ujenzi wa majengo mbalimbali ya shule, Zahanati na Vituo vya Afya, ili kuepuka hasara za kurudia kufanya kazi moja zaidi ya mara moja.

10:1:10:4:1 Ilishauriwa kwamba, Mkurugenzi Mtendaji awe anamwezesha gari Mhandisi wa Ujenzi kwa ajili ya kupita kukagua miradi ya ujenzi.

10:1:10:4:2 Ilielezwa kwamba, ushauri umepokelewa na utazingatiwa kwa utekelezaji.

10:1:10:5 Kuhusu tofali za saruji kutumika katika miradi ya ujenzi wa majengo ya umma, iliulizwa ni lazima kutumia tofali hizo, je, tofali za kuchoma haziwezikutumika katika ujenzi wa majengo ya umma.

10:1:10:5:1 Ilifahamishwa kwa wajumbe kwamba, kutumia tofali za saruji katika ujenzi wa majengo ya umma si lazima, changamoto inayopelekea kulazimika kutumia tofali hizo, ni kukosekana kwa uhakika wa kupata tofali za kuchoma za kutosha kutumika katika ujenzi wa majengo yote ya umma. Kinachozingatiwa katika ujenzi wa majengo ya umma ni ubora wa uimara wa tofali.

10:1:10:6 Kuhusu tofali nyingi za saruji zinazopelekwa kwenye miradi ya ujenzi kutokuwa na ubora na imara, pia kununuliwa kutoka mbali na maeneo ambayo majengo ya umma yanajengwa, wajumbe walijadili na kushauri kwamba, ili kutatua changamoto hizo, Halmashauri ianzishe kiwanda cha kutengeneza tofali, ili kutoa huduma hiyo na kuongeza mapato ya Halmashauri.

10:1:10:6:1 Ilishauriwa kwamba, Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kupitia vikao vyake ijadili kwa kina ajenda ya umuhimu wa Halmashauri kuanzisha kiwanda cha kutengeneza tofali za saruji zenye viwango vya ubora unaotokana na usimamizi wa karibu wa utengenezaji wa tofali hizo ili zitumike katika ujenzi wa majengo ya umma.

10:1:10:6:2 Ilifafanuliwa kwa wajumbe kwamba, ajenda ya uanzishwaji wa kiwanda cha kutengeneza tofali cha Halmashauri, ilishajadiliwa kwenye vikao vya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango na kuazimiwa Halmashauri ipendekeze eneo la kuwekeza mradi huo, ambapo Menejimenti ilifanyia kazi na kuwasilisha mapendekezo hayo kwenye Kamati, na Kamati iliridhia eneo moja la Ufwala yalipo majengo yaliyokuwa yanatumiwa na HIMA.

10:2 **Mrejesho wa Bajeti ya Halmashauri kwa shughuli za maendeleo na matumizi ya kawaida kwa mwaka 2021/2022 baada ya kuidhinishwa na Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI)** ulisomwa na kuwasilishwa kwa wajumbe.

10:2:1 Ilielezwa kwamba, Maandalizi ya bajeti yana umuhimu mkubwa kwa Wilaya yetu na nchi nzima kwa ujumla kwa kuwa;

i. Bajeti ni chombo cha kutekeleza sera za nchi na yale yanayotazamiwa kufanyika kwa muda uliopangwa na gharama zinazohusika.
ii. Bajeti ni chombo cha uwajibikaji kwa kuweka wajibu kwa watu wanaohusika na usimamizi wa fedha na programu mbalimbali.
iii. Pia, Bajeti ni chombo cha kutoa mwelekeo wa uchumi kwa vile hutoa viwango vya uwekezaji rasilimali, kudhibiti matumizi katika umma na viwango vya upatikanaji wa fedha na matumizi ya serikali.

10:2:2 Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Ibara ya 135-139) pamoja na Sheria za Serikali za Mitaa (Na. 7 na Na. 9 za mwaka 1982 na marekebisho ya Na.6/1999) zinasisitiza kuandaa na kutekeleza Mipango na Bajeti zinazokidhi vipaumbele vya wananchi waishio katika Halmashauri kwa muda muafaka.

10:2:3 Hivyo, katika kufanikisha maandalizi ya bajeti yenye uwezo wa kuweza kuhudumia sehemu kubwa ya jamii, ni muhimu rasilimali kidogo inayopatikana kugawanywa vizuri na kutumika kwa malengo kusudiwa ili kuboresha huduma zinazotolewa kwa jamii na hatimaye kupunguza umaskini na kukuza uchumi wa wananchi.

10:2:4 Ilifahamishwa kwa wajumbe kwamba, Halmashauri katika maandalizi yake ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 imezingatia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na;

i) Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025;
ii) Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs)
iii) Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) ya mwaka 2020 – 2025,
iv) Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2020/21 - 2024/25).
v) Maagizo mbalimbali ya Viongozi wa Serikali ikiwemo Hotuba ya Mhe. Rais wakati wa Kuzindua Bunge, Novemba 2020.
vi) Vipaumbele vya Halmashauri katika kuboresha huduma kwa Wananchi wake kwa mwaka 2021/22 kupitia Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo katika maeneo yao,
vii) Sera na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali kupitia Taasisi zake (Wizara na Idara zake),
viii) Miongozo ya bajeti iliyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango.

10:2:5 **Kuhusu malengo/vipaumbele vya Halmashauri kwa mwaka 2021/2022**

10:2:5:1 Ilifafanuliwa kwamba, Bajeti ya 2021/2022 imejielekeza katika Vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani kwa kusimamia kikamilifu vyanzo vya mapato vilivyopo na kuibua vyanzo vipya, ikiwa ni pamoja na matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato.
ii. Kuimarisha dhana ya Utawala Bora kwa kusimamia utoaji bora wa huduma na kuzuia rushwa.
iii. Kusimamia utoaji taaluma katika Shule za Msingi na Sekondari na kuwawezesha
iv. Wanafunzi wa darasa la VII kufaulu mitihani ya kuhitimu Elimu ya Msingi na hivyo kuongeza idadi ya Wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka ujao.
v. Kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa kuimarisha miundombinu iliyopo na kuendelea kujenga majengo mapya, kuboresha upatikanaji wa madawa na kuongeza wataalam.
vi. Kuboresha utoaji wa huduma na kupunguza maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI
vii. Kuendeleza kilimo cha matunda, mazao ya kilimo na mifugo na kuboresha masoko ya mazao.
viii. Kuimarisha shughuli za kiuchumi kwa vijana na wanawake kwa kuwawezesha kupata mikopo ya riba nafuu na hivyo kukuza uchumi na kuongeza ajira kupitia sekta binafsi
ix. Kuimarisha ushirikiano uliopo baina ya wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwa ni pamoja na taasisi zisizo za kiserikali (NGOs), Mashirika ya Dini (FBOs) na Taasisi za Kiraia na Kijamii (CBOs).
x. Uhifadhi wa mazingira kwa kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji vinalindwa na kuzuia motokichaa.

10:2:6 **Kuhusu umbile la bajeti ya mwaka 2021/2022**

10:2:6:1 Ilitaarifiwa kwa wajumbe kwamba, baada ya kukamilika kwa mchakato wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/22 na kupitiwa katika vikao mbalimbali vya Halmashauri, Mkoa na Wizara, Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe imeidhinishiwa jumla ya Shs. 42,127,160,130.00 ambapo fedha kwa ajili ya matumizi ya shughuli zisizo za maendeleo ni kiasi cha Shs. 27,223,259,130.00 zikijumuisha Shs. 1,028,007,000.00 za matumizi ya kawaida na Shs 26,195,252,130.00 za mishahara kwa maeneo ya Ruzuku (Fedha toka Serikali kuu). Aidha, kiasi cha Shs. 1,150,540,000.00 zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya kawaida, Shs. 42,460,000.00 kwa ajili ya mishahara kwa maeneo yasiyo ya Ruzuku (Fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri) na kiasi cha Shs.

1,158,108,000.00 kutokana na gharama za uchangiaji wa huduma za Afya na Elimu.

10:2:6:2 Kwa upande wa shughuli za Maendeleo, jumla ya Shs. 12,552,761,299.45 zimetengwa ikiwa kiasi cha Shs. 7,388,860,965.01 fedha toka serikali kuu (Vyanzo vya Ndani), Shs. 3,956,900,334.44 toka kwa wafadhili mbalimbali na jumla ya Shs. 1,207,000,000.00 mchango wa Halmashauri katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo toka vyanzo vyake vya ndani halisi.

10:2:6:3 Ilielezwa kwamba, mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa ikiwa ni Mapato na Matumizi kwa mwaka 2021/22 ni kama unavyoonekana katika majedwali yanayofuata;

**Jedwali 01: Mapato ya Ndani**

| | Maelezo | Kiasi (TShs) |
|---|---|---|
| Makusanyo ya Mapato ya Ndani | Mapato ya ndani kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC) | 1,150,540,000 |
| | Mapato ya ndani kwa Miradi ya Maendeleo (Dev) | 1,207,000,000 |
| | Mapato ya ndani kwa ajili ya Mishahara (PE) | 42,460,000 |
| | **Jumla ya Mapato ya Ndani halisi** | **2,400,000,000** |
| | *Cost Sharing – (NHIF,CHF,User Fee na Secondary School Fees)* | 239,996,000 |
| | *Michango ya Hostels kwa Shule za Sekondari* | 918,112,000 |
| | **Jumla ya Mapato ya Ndani – Vyanzo vingine** | **1,158,108,000** |
| **Jumla ndogo - 1 (Mapato ya Ndani Halisi na Michango ya Afya na Hosteli)** | | **3,558,108,000** |

**Jedwali 02: Mapato ya Ruzuku kwa Matumizi mengineyo kutoka Serikali Kuu**

| Chanzo cha Fedha | Matumizi mengineyo (OC) – Shs | Mishahara (PE) – Shs | Jumla - Shs |
|---|---|---|---|
| Ruzuku ya Serikali Kuu (LGBG) | 1,028,007,000.00 | 26,195,252,130 | 27,223,259,130.00 |
| **Jumla ndogo - 2** | 1,028,007,000.00 | 26,195,252,130 | **27,223,259,130.00** |

**Jedwali 03: Mchanganuo wa Vyanzo kwa Miradi ya Maendeleo**

| Na | Chanzo cha Fedha/Jina la Mradi | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDCF) | 43,090,000 | 0 | 43,090,000 |
| 2 | Elimu Bure Msingi | 666,117,000 | 0 | 666,117,000 |
| 3 | Elimu Bure Sekondari | 787,590,000 | 0 | 787,590,000 |
| 4 | Fedha za Mitihani (Msingi na Sekondari) | 696,869,000 | 0 | 696,869,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Health Sector Busket Fund (HSBF) | 0 | 353,254,000 | 353,254,000 |
| 6 | UNICEF Support | 0 | 106,142,000 | 106,142,000 |
| 7 | Ujenzi wa Jengo la Utawala | 1,000,000,000 | 0 | 1,000,000,000 |
| 8 | Ujenzi wa Madarasa – Elimu Msingi | 112,500,000 | 0 | 112,500,000 |
| 9 | Ujenzi wa Madarasa – Elimu Sekondari | 112,500,000 | 0 | 112,500,000 |
| 10 | Ukamilishaji wa Zahanati | 150,000,000 | 0 | 150,000,000 |
| 11 | Ukamilishaji wa Kituo cha Afya | 300,000,000 | 0 | 300,000,000 |
| 12 | Ujenzi wa wodi katika Hospitali ya Wilaya | 800,000,000 | 0 | 800,000,000 |
| 13 | Kusaidia Ujenzi wa Maabara - Sekondari | 150,000,000 | 0 | 150,000,000 |
| 14 | TASAF Programme | 0 | 2,258,034,000 | 2,258,034,000 |
| 15 | Mapambano dhidi ya UKIMWI (G/Fund) | 0 | 13,234,000 | 13,234,000 |
| 16 | SEQUIP Programme for Secondary Schools | 0 | 1,585,200,000 | 1,585,200,000 |
| 17 | RSSH | 0 | 25,000,000 | 25,000,000 |
| 18 | National Sanitation Campaign | 0 | 24,000,000 | 24,000,000 |
| 19 | Miradi ya EP4R – Elimu ya Msingi | 0 | 346,581,500 | 346,581,500 |
| 20 | Miradi ya EP4R – Elimu ya Sekondari | 0 | 346,581,500 | 346,581,500 |
| 21 | GPE Lanes | 0 | 64,510,000 | 64,510,000 |
| 22 | C4D | 0 | 22,987,000 | 22,987,000 |
| 23 | NTD's / EAST | 0 | 15,549,000 | 15,549,000 |
| 24 | Support to end Malaria (Malaria fund) | 0 | 2,827,000 | 2,827,000 |
| | **Jumla Ndogo 3** | 7,388,861,000 | 3,956,900,000 | **11,345,761,000** |
| | **JUMLA KUU – MAPATO YOTE** | | | **42,127,160,130** |

**MCHANGANUO WA MATUMIZI YOTE**

**Jedwali Na.1: Mgawanyo wa fedha za Ruzuku toka Serikali kuu kwa kila Idara**

| Vote No | Idara | Mishahara | OC | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 500B | Utumishi | - | 64,260,000.00 | 64,260,000.00 |
| 500A | Utawala | 2,469,007,935.00 | 360,013,000.00 | 2,829,020,935.00 |
| 501A | Mazingira | - | 6,500,000.00 | 6,500,000.00 |
| 502E | Biashara | - | 6,500,000.00 | 6,500,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 503B | Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji | - | 20,000,000.00 | 20,000,000.00 |
| 506D | Ushirika | - | 6,500,000.00 | 6,500,000.00 |
| 512A | Ardhi | - | 6,500,000.00 | 6,500,000.00 |
| 512F | Maliasili | - | 6,500,000.00 | 6,500,000.00 |
| 515A | Ukaguzi wa Ndani | - | 9,000,000.00 | 9,000,000.00 |
| 519A | Nyuki | - | 6,500,000.00 | 6,500,000.00 |
| 527A | Maendeleo ya Jamii | - | 6,500,000.00 | 6,500,000.00 |
| 505A | TEHAMA | - | 4,500,000.00 | 4,500,000.00 |
| 502A | Fedha na Biashara | - | 13,000,000.00 | 13,000,000.00 |
| 506A | Mifugo na Uvuvi | 487,305,180.00 | 12,898,000.00 | 500,203,180.00 |
| 507B | Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | 474,788,025.00 | 13,348,000.00 | 488,136,025.00 |
| 509A | Elimu Msingi | 10,962,766,800.00 | 35,446,000.00 | 10,998,212,800.00 |
| 508A | Elimu Sekondari | 6,792,278,985.00 | 29,618,000.00 | 6,821,896,985.00 |
| 508F | Afya – Utawala (CHMT) | 72,572,600.00 | 78,285,000.00 | 150,857,600.00 |
| 508D | Afya – Kinga | 504,397,620.00 | - | 504,397,620.00 |
| 508E | Vituo vya Afya | 1,093,173,165.00 | - | 1,093,173,165.00 |
| 510B | Zahanati | 2,419,817,400.00 | - | 2,419,817,400.00 |
| 511A | Maji | - | - | - |
| 517A | Ujenzi | 146,707,740.00 | 18,772,000.00 | 165,479,740.00 |
| | **JUMLA** | **26,195,252,130** | **1,028,007,000.00** | **27,223,259,130.00** |

**Jedwali Na 2: Mgawanyo wa fedha za Mapato ya Ndani kwa Idara/Kitengo**

| **Kifungu** | **Idara / Kitengo** | **Mishahara** | **Matumizi Mengineyo** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| 500A | Utawala | 42,460,000 | 757,540,000 | 800,000,000 |
| 501C | Usafi na Mazingira | 0 | 8,000,000 | 8,000,000 |
| 502 (A,B) | Fedha na Biashara | 0 | 140,000,000 | 140,000,000 |
| 503A | Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji | 0 | 35,000,000 | 35,000,000 |
| 505A | Mifugo na Uvuvi | 0 | 15,000,000 | 15,000,000 |

| Kifungu | Idara / Kitengo | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 506A | Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | 0 | 25,000,000 | 25,000,000 |
| 512 (C&E) | Ardhi na Maliasili | 0 | 20,000,000 | 20,000,000 |
| 514A | Sheria | 0 | 8,000,000 | 8,000,000 |
| 515A | Mkaguzi wa Ndani | 0 | 10,000,000 | 10,000,000 |
| 516 (A & B) | Ugavi na Manunuzi | 0 | 25,000,000 | 25,000,000 |
| 517B | Uchaguzi | 0 | 20,000,000 | 20,000,000 |
| 518A | TEHAMA | 0 | 35,000,000 | 35,000,000 |
| 527A | Maendeleo ya Jamii | 0 | 12,000,000 | 12,000,000 |
| 519A | Nyuki | 0 | 10,000,000 | 10,000,000 |
| 507B | Elimu Msingi | 0 | 15,000,000 | 15,000,000 |
| | Elimu Sekondari | 0 | 5,000,000 | 5,000,000 |
| | Ujenzi | 0 | 10,000,000 | 10,000,000 |
| **Jumla Ndogo ya Mapato ya Ndani (60%)** | | **42,460,000** | **1,150,540,000** | **1,193,000,000** |
| **40% Kuchangia Miradi ya Maendeleo** | | | **1,207,000,000** | **1,207,000,000** |
| **Kuchangia Huduma za Afya na Elimu (Ada ya utumiaji wa huduma)** | | | 239,996,000.00 | 239,996,000.00 |
| **Michango ya Hostel kwa Sekondari** | | | 918,112,000.00 | 918,112,000.00 |
| **JUMLA KUU YA MATUMIZI KWA MAPATO YA NDANI** | | | | **3,558,108,000** |

**Jedwali Na.3: Mchanganuo wa fedha za Miradi ya Maendeleo**

| Na | Chanzo cha Fedha/Jina la Mradi | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDCF) | 43,090,000 | 0 | 43,090,000 |
| 2 | Elimu Bure Msingi | 666,117,000 | 0 | 666,117,000 |
| 3 | Elimu Bure Sekondari | 787,590,000 | 0 | 787,590,000 |
| 4 | Fedha za Mitihani (Msingi na Sekondari) | 696,869,000 | 0 | 696,869,000 |
| 5 | Health Sector Busket Fund (HSBF) | 0 | 353,254,000 | 353,254,000 |
| 6 | UNICEF Support | 0 | 106,142,000 | 106,142,000 |
| 7 | Ujenzi wa Jengo la Utawala | 1,000,000,000 | 0 | 1,000,000,000 |
| 8 | Ujenzi wa Madarasa – Elimu Msingi | 112,500,000 | 0 | 112,500,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9 | Ujenzi wa Madarasa – Elimu Sekondari | 112,500,000 | 0 | 112,500,000 |
| 10 | Ukamilishaji wa Zahanati | 150,000,000 | 0 | 150,000,000 |
| 11 | Ukamilishaji wa Kituo cha Afya | 300,000,000 | 0 | 300,000,000 |
| 12 | Ujenzi wa Wodi katika Hospitali ya Wilaya | 800,000,000 | 0 | 800,000,000 |
| 13 | Kusaidia Ujenzi wa Maabara - Sekondari | 150,000,000 | 0 | 150,000,000 |
| 14 | TASAF Programme | 0 | 2,258,034,000 | 2,258,034,000 |
| 15 | Mapambano dhidi ya UKIMWI (G/Fund) | 0 | 13,234,000 | 13,234,000 |
| 16 | SEQUIP Programme for Secondary Schools | 0 | 1,585,200,000 | 1,585,200,000 |
| 17 | RSSH | 0 | 25,000,000 | 25,000,000 |
| 18 | National Sanitation Campaign | 0 | 24,000,000 | 24,000,000 |
| 19 | Miradi ya EP4R – Elimu ya Msingi | 0 | 346,581,500 | 346,581,500 |
| 20 | Miradi ya EP4R – Elimu ya Sekondari | 0 | 346,581,500 | 346,581,500 |
| 21 | GPE Lanes | 0 | 64,510,000 | 64,510,000 |
| 22 | C4D | 0 | 22,987,000 | 22,987,000 |
| 23 | NTD's / EAST | 0 | 15,549,000 | 15,549,000 |
| 24 | Support to end Malaria (Malaria fund) | 0 | 2,827,000 | 2,827,000 |
| | **Jumla Ndogo 3** | 7,388,861,000 | 3,956,900,000 | **11,345,761,000** |
| | **JUMLA KUU – MATUMIZI** | | | **42,127,160,130** |

10:2:7 Ilifafanuliwa kwa wajumbe kwamba, pamoja na majedwali hayo yanayoonesha mgawanyo wa fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa Shughuli za Miradi ya Maendeleo kwa kila Idara/Kitengo, Majedwali mengine yaliyoambatishwa yanaonesha Miradi ya Maendeleo ambayo Halmashauri itatekeleza katika mwaka 2021/22, majedwali hayo yapo kuanzia ukurasa wa 8 hadi 17 wa taarifa iliyowasilishwa.

10:2:3 Wajumbe walipokea na kuridhia kwa utekelezaji taarifa ya Mrejesho wa Bajeti ya Halmashauri kwa shughuli za maendeleo na matumizi ya kawaida kwa mwaka 2021/2022, baada ya kuidhinishwa na Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI).

10:2:4 Wajumbe walishukuru kuwasilishiwa taarifa ya mrejesho wa bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

10:3 **Taarifa ya Rasimu ya Sheria Ndogo ya Uanzishwaji wa Mfuko wa Elimu 2021 katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe,** ilisomwa na kuwasilishwa kwa wajumbe.

10:3:1 Ilifafanuliwa kwa wajumbe kwamba, sheria hii inatungwa kwa mujibu wa Kifungu cha 153 cha Sheria ya Serikali za Mitaa Namba 287 ya Mwaka 1982 Marejeo ya Mwaka 2002. Aidha, **ilikumbushwa** kwamba, uandaaji wa Sheria Ndogo hii unatokana na azimio la kikao cha Wadau wa Elimu Wilaya ya Wanging'ombe la uhitaji wa kuwa na Sheria hii.

10:3:2 Ilifahamishwa kwamba, katika hatua ya awali Sheria Ndogo zimewasilishwa katika ngazi ya Kata ili zijadiliwe kwenye vikao vya Kamati za Maendeleo za Kata.

10:3:3 Wajumbe walipokea na kupitia rasimu hiyo ukurasa kwa ukurasa na kifungu kwa kifungu.

10:3:4 Wajumbe waliridhia na kupitisha kwamba, Halmashauri iendelee na mchakato wa kukamilisha upatikanaji wa Sheria Ndogo ya Uanzishwaji wa Mfuko wa Elimu 2021 katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.

10:4 **Mapendekezo ya ratiba ya vikao kwa mwaka wa fedha 2021/2021** yalisomwa na kuwasilishwa kwa wajumbe.

10:4:1 Wajumbe walipokea na kupitia rasimu ya ratiba hiyo na kupitisha. Ilishauriwa na kusisitizwa kwamba, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ratiba ya vikao ifuatwe na kutekelezwa kama ilivyoidhinishwa na Baraza la Madiwani.

**MUHTASARI NA. WDC/MBM/11/08/2021/2022 – TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI YA MAENDELEO KUTOKA SEKTA ZINGINE ZA SERIKALI NDANI YA HALMASHAURI, ZILIZOALIKWA KUWASILISHA TAARIFA ZAKE KWENYE MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 06.08.2021**

11:1 **Taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na TARURA kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021 robo ya nne (IV) kwa mwaka wa fedha 2020/2021,** ilisomwa na kuwasilishwa kwa wajumbe.

11:1:2 Wajumbe walipokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za TARURA na kuwasilisha changamoto mbalimbali zinazohusiana na miundombinu ya barabara na madaraja katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri kwa Meneja wa TARURA.

11:1:3 Baada ya changamoto zote kupokelewa, ilishauriwa kila Mheshimiwa Diwani awasiliane na Meneja wa TARURA kuelezea barabara/daraja inayohitaji matengenezo ili aweze kufanyia kazi.

11:1:4 Ushauri ulipokelewa kwa utekelezaji.

11:1:5 Wajumbe walipitisha taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na TARURA kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021 robo ya nne (IV) kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

11:2 **Taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na RUWASA kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021 robo ya nne (IV) kwa mwaka wa fedha 2020/2021,** ilisomwa na kuwasilishwa kwa wajumbe.

11:2:1 Wajumbe walipokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za RUWASA na kujadili:

11:2:2 **Majadiliano**

11:2:2:1 Kuhusu mradi wa maji Igando – Kijombe, iliulizwa hadi sasa mradi huo umekamilika kwa asilimia ngapi? Kwa nini katika taarifa ya mradi huo haijaelezwa mkakati wa utekelezaji wa mradi huo?

11:2:2:2 Ilifafanuliwa kwa wajumbe kwamba, mradi huo ulisanifiwa kwa vijiji 10, ukubwa wa mradi umepelekea mradi huo utekelezwa kwa awamu, awamu ya kwanza, unatekelezwa kwa vijiji vya Malangali na Hanjawanu, awamu ya pili ambayo itatekelezwa kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 vimeongezwa vijiji 2.

11:2:2:3 Ilifahamishwa kwa wajumbe kwamba, changamoto iliyopo kwa sasa katika utekelezaji wa mradi wa maji Igando – Kijombe ni mkandarasi kutolipwa fedha za kazi alizofanya za awali katika mradi huo. Ameahidi kuendelea na kazi baada ya kulipwa fedha anazodai.

11:2:2:4 Ilielezwa kwamba, mkakati uliopo ni kuendelea kuongeza vijiji 2 kwa kadri fedha zinavyopatikana za utekelezaji wa mradi huo.

11:2:2:5 Ilitaarifiwa kwa wajumbe kwamba, Mkoa umelichukua suala la mradi wa maji Igando – Kijombe kwa ajili ya msukomo zaidi ili mradi huo uweze kufanikiwa kutekelezwa.

11:2:2:6 Wajumbe walishauri kwamba, Halmashauri ishiriki katika kuchukua hatua za ziada zaidi za ufuatiliaji, ili kuhakikisha mradi huo unakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

11:2:2:7 Wajumbe walipitisha taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na RUWASA kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021 robo ya nne (IV) kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

11:3 **Taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na WANGIWASA kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021 robo ya nne (IV) kwa mwaka wa fedha 2020/2021,** ilisomwa na kuwasilishwa kwa wajumbe.

11:3:1 Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili.

11:3:2 **Majadiliano**

11:3:2:1 Kuhusu mradi wa maji unaofadhiliwa na India, iliulizwa mradi huo utaanza kutekelezwa lini? Ili kuondoa kero ya wananchi kukosa maji.

11:3:2:1:1 Ilifahamishwa kwa wajumbe kwamba, Wakandarasi wa kutekeleza mradi huo, wameshapatikana, kuanzia mwezi Septemba, 2021 mradi huo utaweza kuanza kutekelezwa.

11:3:2:2 Kuhusu changamoto iliyowasilishwa na WANGIWASA ya Paroko - Luduga kuingili Mamlaka kwa kusambaza maji kwa wananchi na kwamba mamlaka inataka kuchukua jukumu la kufunga maji hayo yasipelekwe kwa wananchi, wajumbe walijadili kwa kina changamoto hiyo na kushauri yafuatayo:

i. Kwa sababu huduma ya maji inahitajika sana kwa wananchi, WANGIWASA watambue huduma ya paroko kwa wananchi, ili wananchi waendelee kupata huduma ya maji.
ii. WANGIWASA wafanye mawasiliano na Paroko Luduga, ili wakatazame usalama wa chanzo cha maji na kupima maji hayo, ili kuhakiki usalama wa maji hayo na kuwaepusha wananchi kutumia maji yenye madini hatarishi kwa afya ya binadamu, kama madini aina ya zebaki.
iii. WANGIWASA waandike barua ya kumpongeza Paroko – Luduga kusaidia kusambaza huduma ya maji kwa wananchi. Katika barua hiyo, apewe angalizo la kutoa taarifa kwa Mamlaka zilizopo kisheria, kwa ajili ya kutoa huduma ya maji kwa wananchi, hususani WANGIWASA yenye dhamana katika eneo husika.
iv. Kwa ujumla ilisisitizwa kwamba, huduma ya maji anayoitoa Paroko – Luduga isisitishwe, WANGIWASA na Paroko wote waendelee kuwapatia huduma ya maji wananchi.

11:3:2:3 Baada ya majadiliano hayo, wajumbe waliridhia taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na WANGIWASA kwa kipindi cha kuishia mwezi Juni, 2021.

11:4 Taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na TANESCO kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021 robo ya nne (IV) kwa mwaka wa fedha 2020/2021, haikuwasilishwa kutokana na taasisi hiyo kutokuwa na mwakilishi aliyehudhuria mkutano huo.

**MUHTASARI NA. WDC/MBM/12/08/2021/2022 – MASUALA YA KIUTUMISHI**

12:1 **Mashauri ya Kinidhamu ya Watumishi**

12:1:1 Ilitaarifiwa kwa wajumbe kwamba, kuna mashauri kumi (10) ya kinidhamu ya Watumishi ambao wameenda kinyume na maadili ya kazi kwa kufanya makosa mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye jedwali ikiwa na mapendekezo ya Kamati ya Wataalam na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango;

| S/N | JINA | CHEO | TUHUMA/ SHITAKA LINALOMKABILI | HATUA ZA AWALI ZILIZOCHUKULIWA NA MENEJIMENTI | UTETEZI WAKE | MAPENDEKEZO YA MENEJIMENTI | MAPENDEKEZO YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO | MAAMUZI YA BARAZA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Fadhili Abdallah Mkata | Mtunza Kumbukumbu Msaidizi II | Utoro kazini wa zaidi ya siku tano (5) mfululizo kuanzia tarehe 13/12/2020 hadi 23/12/2020. | -Tarehe 13/01/2021 Mkurugenzi Mtendaji alimwandikia notice yenye Kumb. Na. WDC/SC.20/1/VOL.II/12 na Hati ya Mashtaka kwa barua yenye Kumb. Na. WDC/SC.20/1/ VOL. II/13.<br><br>-Alisimamishwa kazi kwa tuhuma za kutenda kosa la Jinai Barua Kumb. Na. WAG/CID/C.S/4/4/122, Barua Kumb. Na. PCF.236/2 ya tarehe 26 Januari 2021. | Alikiri kosa la utoro wa zaidi ya siku tano (5) kutokana na yeye kuwa na matatizo ya kijamii, alishikiriwa na Polisi na hakuwa na simu ya kuweza kutoa taarifa. | -Menejimenti inasubiri hitimisho la kesi yake ya Jinai NG.WAG/IR/493/2020 ili iweze kuendelea na shauri lake la kinidhamu, Kanuni ya 50 (b) ya mwaka 2003 inataka Mamlaka ya Nidhamu kutokuendelea na Hatua zozote mpaka kukamilika kwa mwenendo wa kesi ya Jinai.<br><br>-Endapo kesi hiyo ikiisha kwa sababu za kiufundi Mwajiri hazuiliwi kumchukulia hatua za Kinidhamu kwa kesi hiyo hiyo. Kanuni Na. 50 (c) ya Kanuni za Utumishi wa Umma<br>- Pia Menejimenti inashauri (Kanuni ya 39 (2) itumike. Barua ya kusimamishwa kazi ya awali bila kuathiri mshahara wake (Ifutwe) apewa barua nyingine yenye adhabu kutopewa mshahara wote. Ila sehemu ya Mshahara ambayo ni 1/3 ya mshahara wake hadi hapo shauri lake litakapohitimishwa. | Asimamishwe kazi na kupewa sehemu ya mshahara ambayo ni 1/3 ya Mshahara wake hadi hapo shauri lake litakapohitimishwa na Mahakama. | Asimamishwe kazi na kupewa sehemu ya mshahara ambayo ni 1/3 ya Mshahara wake hadi hapo shauri lake litakapohitimishwa na Mahakama |
| S/N | JINA | CHEO | TUHUMA/ SHITAKA LINALOMKABILI | HATUA ZA AWALI ZILIZOCHUKULIWA NA MENEJIMENTI | UTETEZI WAKE | MAPENDEKEZO YA MENEJIMENTI | MAPENDEKEZO YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO | MAAMUZI YA BARAZA |
| 2 | Maduka Michael Kitaponda | Mfamasia Daraja la II | Kutokuwepo kazini zaidi ya siku tano mfululizo bila ruhusa au sababu za msingi zinazotambuliwa na Mwajiri. Kanuni ya 57 (i) sambamba na aya ya nne (4) ya sehemu A ya jedwali la kwanza katika Kanuni Na. 42 ya Kanuni za mwaka 2003 za utumishi wa Umma, kuanzia tarehe 17/01/2021 | Alifunguliwa Hati ya Mashtaka kwa barua yenye Kumb. Na. WDC/CS.20/1/3/65 ya tarehe 27/05/2021 na kupewa notisi WDC/CS.20/1/3/65.<br><br>Kwa mujibu wa Kanuni Na. 44 (3) za Utumishi wa Umma baada ya yenye kuandika notisi ya kuacha kazi ndani ya masaa 24 bila kuzingatia matakwa ya Kanuni 42 (i) | | kwa kuwa utoro wa Mtumishi huyu ni wa muda mrefu zaidi ya siku tisini (90) na hakuna mawasiliano yoyote yanayofanyika na Mtumishi huyu. Menejimenti inashauri hatua kali za Kinidhamu zichukuliwe dhidi yake kwa kuzingatia Kanuni 42 (i) ya Kanuni za Utumishi | Afukuzwe kazi, Taratibu za Kiutumishi zizingatiwe . | Afukuzwe kazi, Taratibu za Kiutumishi zizingatiwe . |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | hadi sasa. Mtumishi huyu aliandika barua ya kuomba kuacha kazi masaa 24 tarehe 17/01/2021 bila kuwasilisha Hati ya malipo ya Mshahara ghafi (Basic salary) na kupewa idhini kwa maandishi ya kuacha kazi toka kwa Mwajiri kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 toleo la tatu Kifungu 49 (4). | inayomtaka Mtumishi kulipa mshahara wa mwezi mmoja. (Basic Salary) kwa Mwajiri wake ili kupata kibali cha kuacha kazi masaa 24, Alipaswa kuzingatia matakwa ya Kanun za kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 kipengele F.49 (4). | | wa Umma za mwaka 2003 na marekebisho yake barua Kumb. Na. CAC.228/257/01"A" 125 ya tarehe 10/01/2020. Ambapo adhabu ni kufukuzwa kazi, kushushwa cheo ama kukatwa asilimia 15% ya mshahara kwa miaka mitatu. Menejimenti inashauri afukuzwe kazi. | | |
| **S/N** | **JINA** | **CHEO** | **TUHUMA/ SHITAKA LINALOMKABILI** | **HATUA ZA AWALI ZILIZOCHUKULIWA NA MENEJIMENTI** | **UTETEZI WAKE** | **MAPENDEKEZO YA MENEJIMENTI** | **MAPENDEKEZO YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO** | **MAAMUZI YA BARAZA** |
| 3 | Suleiman Gasto Bundala | Tabibu Msaidizi | Kutokuwepo kazini zaidi ya siku tano mfululizo bila ruhusa au sababu za msingi zinazotambuliwa na Mwajiri Kanuni ya 57 (i) sambamba na aya ya 4 ya sehemu A ya Jedwali la kwanza katika Kanuni Na. 42 ya Kanuni za mwaka 2003 za Utumishi wa Umma, kuanzia tarehe 31 Oktoba 2020 alipotakiwa kuripoti kituo chake cha kazi baada ya kuhitimu masomo yake "Clinical Officer" Kwamba mtumishi tajwa aliajiriwa tarehe 23/07/2018 kama Tabibu Msaidizi na kupangiwa kufanya kazi katika Zahanati ya Malangali Oktoba 2019 na kupewa ruhusa ya kwenda masomoni kwa kipindi cha mwaka mmoja 2019/2020 hadi leo hii hayupo kazini. | Aliandikiwa hati ya Mashtaka Barua Kumb. Na. WDC/CS.20/1/3/05 ya tarehe 23 April, 2021 baada ya Mganga Mkuu (W) kumtaarifu Mwajiri wake. Kwa kuwa utoro wake ni wa muda mrefu na kwa kuwa ruhusa yake ilifikia ukomo tarehe 31 Oktoba 2020 na kutoripoti katika kituo chake cha kazi bila ruhusa wala sababu za msingi kwa zaidi ya siku 150. | | kwa kuwa utoro wa Mtumishi huyu ni wa muda mrefu zaidi ya siku tisini (90) na hakuna mawasiliano yoyote yanayofanyika na Mtumishi huyu. Menejimenti inashauri hatua kali za Kinidhamu zichukuliwe dhidi yake kwa kuzingatia Kanuni 42 (i) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na marekebisho yake barua Kumb. Na. CAC.228/257/01"A" 125 ya tarehe 10/01/2020. Ambapo adhabu ni kufukuzwa kazi, kushushwa cheo ama kukatwa asilimia 15% ya mshahara kwa miaka mitatu. Menejimenti inashauri afukuzwe kazi. | Afukuzwe kazi | Afukuzwe kazi |
| **S/N** | **JINA** | **CHEO** | **TUHUMA/ SHITAKA LINALOMKABILI** | **HATUA ZA AWALI ZILIZOCHUKULIWA NA MENEJIMENTI** | **UTETEZI WAKE** | **MAPENDEKEZO YA MENEJIMENTI** | **MAPENDEKEZO YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO** | **MAAMUZI YA BARAZA** |
| 4. | Elly Mpogolo | Mtendaji wa Kijiji Daraja III | Utoro kazini tangu 07/01/2021 hadi 13/01/2021 tarehe ya kuandikiwa Mashtaka. | Alifunguliwa Hati ya Mashtaka ya Tarehe 13/02/2021 yenye Kumb. Na. WDC/CS.20/1/Vol. II/11 kwa | | Kwa kuwa utoro wa Mtumishi huyu ni wa muda mrefu na kwa kuwa Kamati ya awali ya Uchunguzi | Afukuzwe kazi | Afukuzwe kazi |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Shitaka la kwanza – Utoro zaidi ya siku tano kukiuka Kanuni Na. 57 (i) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2003 sambamba na sehemu A Kipengele cha nne cha Kanuni Na. 42 Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Ikisomwa pamoja na Kanuni F. 27 (d) ya Kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 toleo la tatu. Kwa kutokuwepo kituo chake cha kazi kuanzia tarehe 07/01/2021 hadi tarehe 13/01/2021 siku tarehe ya kuandikiwa kwa Hati ya Mashtaka na kuwa na jumla ya siku saba (7).<br><br>Shitaka la pili – Ubadhilifu wa fedha za Umma kiasi cha TSh. 55,000/= kwa ajili ya ujenzi wa darasa la shule ya Sekondari Thomasi Nyimbo. Pamoja na kutokuwasilisha vitabu vilivyotumika kukusanya michango na kutenda kosa kwa mujibu wa Kifungu Na. 42 cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. | Mujibu wa Kanuni Na. 44 (3) za Utumishi wa Umma .<br><br>Tarehe 13/01/2021 Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri alimsimamisha kazi kwa barua yenye Kumb. Na. WDC/CS.20/1/Vol.II/9.<br><br>-Tarehe 04/05/2021 Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe aliteua Kamati ya Uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili Mtendaji wa Kijiji Daraja III Elly Mgolo. Kwa barua yenye Kumb. Na. WDC/CS.20/1/Vol.11/26 , WDC/CS.20/11/25, WDC/CS.20/I/Vol. 11/24 na WDC/CS.20/I/Vol.11/23 za tarehe 04/05/2021. | | imethibitisha utoro wa Mtumishi Elly Mpogolo kuanzia Tarehe 01/01/2021 hadi tarehe 15/02/2021. Menejimenti inashauri afukuzwe kazi kwa mujibu wa Kanuni Na. 42 (i) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2003. | | |
| **S/N** | **JINA** | **CHEO** | **TUHUMA/ SHITAKA LINALOMKABILI** | **HATUA ZA AWALI ZILIZOCHUKULIWA NA MENEJIMENTI** | **UTETEZI WAKE** | **MAPENDEKEZO YA MENEJIMENTI** | **MAPENDEKEZO YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO** | **MAAMUZI YA BARAZA** |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 5 | Maulidi Ramadhani Kasitu | Mtendaji wa Kijiji cha Banawanu | Upotevu wa fedha za Umma kiasi cha TSh. 1.559,800/= ikiwa ni fedha za makusanyo ya michango ya shule ya Msingi Banawanu, Kinyume na dhamira au tabia njema ya Utumishi wa Umma Kanuni Na. 42 jedwali la sehemu A Kipengere cha 1 cha makosa mazito. | Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Wanging'ombe alimsimamisha kazi kwa barua yenye Kumb. Na. WDC/CS.20/1/ Vol. II/8 ya tarehe 03/12/2020.<br><br>Tarehe 04/12/2020 Mkurugenzi Mtendaji aliwandikia notisi kwa barua yenye Kumb. Na. WDC/SC.20/I/Vol. II/8 pia alimwandikia Hati ya Mashtaka yenye Kumb. Na. WDC/CS.20/1/Vol.II/8 ya tarehe 01/01/2021.<br><br>Mnamo tarehe 22/04/2021 Mkurugenzi Mtendaji Wilaya alimpumzisha majukumu kwa barua yenye Kumb. Na. WDC/CS.20/1/VOL.II/14 . | | Mpaka sasa amerejesha kiasi cha TShs. 1,260,000/= bado 339,800/= Menejimenti inashauri asamehewe kwa kuwa amekiri kosa na ameonyesha Mwitikio wa kuendelea kurejesha kiasi alichotumia bila idhini ya Mamlaka.<br><br>-Apewe Karipio kali na kurejesha kazini hata hivyo anakaribia kustaafu. | Apewe karipio kali na kurejeshwa kazini baada kulipa deni lake kwa kuwa ameonesha nia thabiti ya kulipa deni. | Apewe karipio kali na kurejeshwa kazini baada kulipa deni lake kwa kuwa ameonesha nia thabiti ya kulipa deni. Aidha, kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia tarehe 06.08.2021 awe amerejesha kiasi cha fedha anazodaiwa. |
| **S/N** | **JINA** | **CHEO** | **TUHUMA/ SHITAKA LINALOMKABILI** | **HATUA ZA AWALI ZILIZOCHUKULIWA NA MENEJIMENTI** | **UTETEZI WAKE** | **MAPENDEKEZO YA MENEJIMENTI** | **MAPENDEKEZO YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO** | **MAAMUZI YA BARAZA** |
| 6 | Steven B. Mwasongela | Muuguzi Daraja I, Kituo cha Afya Palangawanu (kuanzia Tar. 01 Juni 2021) | Utoro kazini wa zaidi ya siku tano mfululizo kuanzia tarehe 22/06/2020 hadi tarehe 23/03/2021 siku ya kuandikwa kwa hati ya Mashtaka bila sababu za Msingi zinazotambuliwa na Mwajiri zilizomuzuia kuripoti kituo kipya cha kazi , Kanuni ya 57 ya Sehemu "A" ya Jendwali la kwanza katika Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. | - Aliandikiwa barua Kumb. Na. WDC/CS.20/3/57/ ya Hati ya Mashtaka kumtaka ajieleze baada ya Mganga Mfawidhi wa kituo taarifa.<br><br>- Baada ya utetezi wake kutia mashaka majiri aliunda Kamati ya Uchunguzi wa Tuhuma za uroto zinazomkabili baada ya Mtumishi kukana Mashtaka yote.<br><br>Alisimamishwa mshahara wake kuepuka hoja ya mishahara hewa na hasara kwa Serikali. | Mnamo Tarehe 05/04/2021 alimuandikia Mwajiri barua ya utetezi juu ya Mshataka mawili (2) yaliyokuwa yamamkabili ya utoro na kukiuka maadili ya Utumishi wa Umma na kukana Mashtka yake yote. | Kwa kuwa tuhuma za utoro zimethibitishwa na Kamati ya awali iliyokwenda kituo cha Afya Palangawanu tarehe 20/07/2021 na kwa kupitia orodha ya mahudhurio kazini, na yeye kukiri kosa mbele ya Kamati kwa Maandishi na kutokana na yeye kugoma kuhamia kituo kipya cha kazi bila kufuata hatua stahiki kama Mtumishi wa Umma.<br><br>Tarehe 20/07/2021 Menejimenti inashauri apewe adhabu ya kushushwa Cheo kwa muda wa miaka mitatu (3) na Mshahara toka cheo cha Muuguzi Daraja la I kuwa Muuguzi **Daraja la II** ikiwa ni matakwa ya Kanuni ya 42 (1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. | Kamati inapendekeza ashushwe cheo na mshahara kutoka cheo cha Muuguzi Daraja la I kuwa Muuguzi Daraja la II kwa muda wa miaka mitatu (3). | Kamati inapendekeza ashushwe cheo na mshahara kutoka cheo cha Muuguzi Daraja la I kuwa Muuguzi Daraja la II kwa muda wa miaka mitatu (3). |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Sambamba na marekebisho yake barua Kumb. Na. CAC.228/257/01"A"/ 125 ya tarehe 10/01/2020 ambapo adhabu ya kwanza ya Kanuni hizi ni kufukuzwa kazi, kushushwa cheo na mshahara (ya pili) ama kukatwa asilimia 15% ya Mshahara kwa muda wa miaka mitatu. | | |
| **S/ N** | **JINA** | **CHEO** | **TUHUMA/ SHITAKA LINALOMKABILI** | **HATUA ZA AWALI ZILIZOCHUKULIWA NA MENEJIMENTI** | **UTETEZI WAKE** | **MAPENDEKEZO YA MENEJIMENTI** | **MAPENDEKEZ O YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO** | **MAAMUZI YA BARAZA** |
| 7 | Fredirick Lufilisha Mihayo | Mteknolojia Msaidizi Dawa – Kituo cha Afya Palangawa nu | Utoro kazini zaidi ya siku tano mfululizo kuanzia tarehe 18/12/2020 alipoondoka kituo chake cha kazi bila ruhusa, mpaka tarehe 03/03/2021 bila sababu za msingi zinazotambuliwa na Mwajiri zilizomzuia kuhamia kituo kipya cha kazi baada ya kupata uhamisho wa kutoka Makao Makuu kwenda kituo cha Palangawanu. Barua Kumb. WDC/PF/592/14 ya tarehe 19/06/2020 kwamba alilipoti kituo kipya tarehe 20/06/2020 akatekeleza majukumu yake hadi tarehe 17/12/2020 .<br><br>Shtaka la pili Kukiuka, maadili na mwenendo mwema wa Utumishi wa Umma kinyume na kipengele cha 14 cha Sehemu "A" ya Jedwali la kwanza la Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. | Barua ya mganga Mfawidhi wa kituo cha Afya, Palangawanu ya tarehe 19/02/2021 isiyo na Kum. Na. ambayo inaelezea utoro wa Mtumishi Fredrick O. Mihayo,anayefanya kazi ya Mteknolojia Dawa.<br><br>-Idara ya Afya, ilifanya jitihada za kumtafuta na ikashindikana kumpata kutokana na kutokuwa na mawasiliano naye.<br><br>-Mnamo Tarehe 23/02/2021 Mganga Mkuu alimwandikia Mwajiri taarifa ya utoro wa Mtumishi Fedrick O. Mihayo kwa ajili ya kuchukua hatua Barua Kumb. Na. PF.592/16.<br><br>-Mnamo tarehe 23/03/2021 aliandikiwa barua Kumb. Na. WDC/CS.20/3/56 ya Hati ya Mashtaka kumtaka ajieleze kuhusiana na Tuhuma za utoro na kukiuka maadili na mwenendo mwema wa Utumishi.<br><br>Kamati ya awali ya uchunguzi kuthibitisha mwenendo wake baada ya kukiri kosa ikiwa ni pamoja na kufika eneo lake la kazi na kufanya mahojiano ya ana kwa ana. | Kupitia Barua yake ya tarehe 6/4/2021 isiyona kumbukumbu namba, alikiri kosa la utoro lililojitokeza na kuahidi kutojirudia tena kwa kosa alilotenda na kuomba msamaha.<br><br>-Katika mahojiano ya ana kwa ana yaliyfanywa kati ya yeye na Mganga mfawidhi wakituo cha Afya Palangawanu na Kamati ya awali ya Uchunguzi wa Mwenendo wake kwa sasa mahali pa kazi aliendelea kukiri kwamba asamehewe hatarudia kuondoka kituo cha kazi bila taarifa na kwamba changamoto zilizokuwa zinamkabili kifamilia zimekwisha tatuliwa. | Kwa kuwa Mtumishi amekiri kosa kupitia barua yake ya tarehe 06/04/2021, na kukiri mbele ya Kamati ya uchunguzi iliyokwenda tarehe 20/07/2021 kujiridhisha na mwenendo wake katika utekelezaji wa majukumu yake - Kwa mujibu Kanuni ya 42 (1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, na marekebisho yake barua Kumb. Na. CAC.228/257/01"A"/ 125 ya tarehe 10/01/2020, ambapo adhabu ya kwanza ni kufukuza kazi ya pili kushushwa cheo na Mshahara ama kukatwa asilimia 15 ya mshahara kwa muda wa miaka mitatu, Menejimenti inashauri apewe adhabu ya kukatwa 15% ya Mshahara wake kwa muda wa miaka mitatu (3). | Apewe Barua ya Onyo, endapo kosa hili litajirudia hatua kali za Kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake. | Apewe Barua ya Onyo, endapo kosa hili litajirudia hatua kali za Kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake |

| S/N | JINA | CHEO | TUHUMA/ SHITAKA LINALOMKABILI | HATUA ZA AWALI ZILIZOCHUKULIWA NA MENEJIMENTI | UTETEZI WAKE | MAPENDEKEZO YA MENEJIMENTI | MAPENDEKEZO YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO | MAAMUZI YA BARAZA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 8 | Goodluck Mbembati | Mtendaji wa Kijiji Daraja la III, Kijiji cha Mtapa Kata ya Igwachanya. | Wizi wa fedha za Umma kiasi cha TShs. 1,305,585.19 ikiwa ni fedha za makusanyo ya Halmashauri. Pesa hizo zilikusanywa katika mashine ya kukusanyia (POS) Ushuru. Iliyopo katika Kijiji cha Mtapa Kata ya Igwachanya kati ya Mwezi wa nane na tisa 2019. | Mkurugenzi Mtendaji alimwandikia Hati ya Mashtaka, Notisi na kumsimamisha kazi, kwa barua yenye Kumb. Na. WDC/CS.20/1/112 ya tarehe 21/10/2021. | Hakujibu hati ya mashtaka. | Kwa kuwa Mtumishi huyu anakabiliwa na kesi ya Jinai Mahakamani kesi Na. 133/2019. Menejimenti inashauri kusubiri kuhitimishwa kwa kesi ya Jinai ndipo kesi ya Nidhamu iendelee. Kanuni Na. 50 (b) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. | Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Menejimenti, kusubiri kuhitimishwa kwa kesi ya Jinai ndipo mashauri ya Nidhamu yaendelee. | Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Menejimenti, kusubiri kuhitimishwa kwa kesi ya Jinai ndipo mashauri ya Nidhamu yaendelee. |
| 9 | Beatus Leonard Mdzovela | Mtendaji wa Kijiji Daraja la III. Kijiji cha Uhenga | Shtaka la kwanza Utoro wa zaidi ya siku tano mfululizo bila taarifa yoyote kwa Mwajiri wake.<br><br>-Shitaka la pili kesi ya Jinai (Mauaji) kesi Na. 10/2020 Wang.IR.162. | Mkurugenzi Mtendaji alimwandikia Mashataka yenye Kumb. Na. WDC/CS.20/I/VOL.II/10 ya tarehe 06/04/2020 na notisi yenye Kumb. Na. WDC/CS.20/I/VOL.II/9 ya tarehe 06/04/2020.<br><br>-Mkurugenzi Mtendaji alimsimamisha kazi kwa barua yenye Kumb. Na. WDC/CF/PF.21/9/28 ya Tarehe 02/09/2020. | Hakujibu hati ya mashtaka. | Kwa kuwa shitaka lake liko Mahakamani kwa kesi ya Jinai. Menejimenti inashauri kusimamishwa kwa mwenendo wa kesi ya nidhamu hadi hapo kesi ya Jinai itakapohitimishwa na afutwe kwenye payroll kuepuka haja ya Mishahara hewa kwa kuwa ni muda mrefu na kesi haijaanza kusikilizwa. | Mtumishi asimamishwe kazi na Mshahara apewe 1/3 ya Mshahara wake hadi hapo kesi yake itakapohitimishwa. | Mtumishi asimamishwe kazi na Mshahara apewe 1/3 ya Mshahara wake hadi hapo kesi yake itakapohitimishwa. |
| 10 | Christina Kelvin Lugome | Mtendaji wa Kijiji Daraja la III. Kijiji cha Ikulimambo | Utoro kazini zaidi ya siku tano mfululizo kuanzia tarehe 21/12/2016 alipoondoka kituo chake cha kazi bila ruhusa, mpaka sasa bila sababu za msingi zinazotambuliwa na Mwajiri | Mkurugezi Mtendaji alimwandikia Mashataka yenye Kumb. Na. WDC/CS.20/1/62 ya tarehe 01/08/2017 na notisi ya tarehe 01/08/2017.<br><br>-Mshahara wa Mtumishi ulisimamishwa kuepuka hoja za mishahara hewa. | Hakujibu hati ya mashtaka. | kwa kuwa utoro wa Mtumishi huyu ni wa muda mrefu zaidi ya miaka mitatu (3) na hakuna mawasiliano yoyote yanayofanyika na Mtumishi huyu. Menejimenti inashauri hatua kali za Kinidhamu zichukuliwe dhidi yake kwa kuzingatia Kanuni 42 (i) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na marekebisho yake barua Kumb. Na. CAC.228/257/01"A" | Afukuzwe Kazi, kutokana na utoro wake kwa muda mrefu. | Afukuzwe Kazi, kutokana na utoro wake kwa muda mrefu. |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 125 ya tarehe 10/01/2020. Ambapo adhabu ni kufukuzwa kazi, kushushwa cheo ama kukatwa asilimia 15% ya mshahara kwa miaka mitatu. Menejimenti inashauri afukuzwe kazi. | | |

12:1:2 Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kupitia mashauri ya kinidhamu yote kumi, kama yalivyowasilisha pamoja na mapendekezo ya Menejimenti na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

12:1:3 Wajumbe walijadili kwa kina kila shauri husika na kufikia maamzi kama ilivyoainishwa kwenye kolamu ya maamuzi ya Baraza la Madiwani katika jedwali hapo juu.

12:1:4 Kuhusu mashauri ya kinidhamu kucheleweshwa kuwasilishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani, ilishauriwa mashauri ya kinidhamu kwa watumishi, yaweyanawasilishwa kwa wakati kwenye vikao vya kisheria ili wajumbe waweze kutoa maamuzi kwa wakati.

12:1:5 Kuhusu Maulidi Ramadhani Kasitu Mtendaji wa Kijiji cha Banawanu Kata ya Udonja, anayedaiwa kumalizia kiasi cha TZS. 339,800/= baada ya kurejesha kiasi cha TZS. 1,260,000/= kati ya TZS. 1.559,800/= alichokuwa anadaiwa, wajumbe walijadili na kuazimia kwamba, kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia tarehe 06.08.2021 mtumishi huyo, awe amerejesha kiasi cha fedha anazodaiwa.

12:1:6 **AZIMIO:** Kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia tarehe 06.08.2021 Bw. Maulidi Ramadhani Kasitu awe amerejesha kiasi chote cha TZS. 339,800/= (fedha anazodaiwa za michango ya wananchi Kijiji cha Banawanu).

**MUHTASARI NA. WDC/MBM/13/08/2021/2022 – KUFUNGA MKUTANO**

13:1 Katibu aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki mkutano huo na kujadili ajenda zote za mkutano.

13:2 Baada ya hapo, alimkaribisha Mwenyekiti aweze kufunga mkutano.

13:3 Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuonesha ushirikiano katika kuzijadili ajenda zote za mkutano huo.

13:4 Aliwashukuru wajumbe kwa kutumia busara na hekima katika kufikia maamuzi sahihi kwa ajenda zote za mkutano.

13:6 Alisisitiza kwamba, wajumbe na watendaji waendelee kuchukua tahadhari ya UVIKO – 19.

13:7 Mwenyekiti alifunga mkutano saa **09:28** alasiri tarehe 06.08.2021 siku ya Ijumaa.

**NAIDHINISHA USAMBAZWE/UPELEKWE KWA WAJUMBE**

..........................................

Maryam A. Muhaji

**Katibu**

Tarehe....22/10/2021

***UMETHIBITISHWA***

.........................................

Ndg. Ferd Y. Mhanze
**Katibu**
Tarehe....................

.........................................

Mhe. Agnetha J. Mpangile
**Mwenyekiti**
Tarehe.......................

**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**

**UTEKELEZAJI WA MAAGIZO/MAAZIMIO YA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 05 – 06/08/2021 SIKU YA ALHAMISI NA IJUMAA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI**

| NA | AZIMIO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | **Muhtasari Na. WDC/MBM/04/08/2021/2022 Dondoo Na. 4:5**<br><br>**AZIMIO:** Mrejesho wa ufumbuzi/utatuzi wa changamoto za kila Kata zilizoainishwa kwenye taarifa zilizowasilishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani tarehe 5.08.2021 uwasilishwe kwenye Kata zote 21 kwa barua (Watendaji wa Kata zote wafahamishwe kwa barua). | Barua Kumb. Na.WDC/C.50/8/108 ya tarehe 27.09.2021 imeandikwa kwa Watendaji wote wa Kata. |
| 2 | **Muhtasari Na. WDC/MBM/12/08/2021/2022 Dondoo Na.12:1:6**<br><br>**AZIMIO:** Kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia tarehe 06.08.2021 Bw. Maulidi Ramadhani Kasitu awe amerejesha kiasi chote cha TZS. 339,800/= (fedha anazodaiwa za michango ya wananchi Kijiji cha Banawanu). | Ameshalipa kiasi chote. |

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**

# MUHTASARI WA MKUTANO MAALUM WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 23.09.2021 SIKU YA ALHAMISI KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI

## HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

## MUHTASARI WA MKUTANO MAALUM WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 23.09.2021 SIKU YA ALHAMISI KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Agnetha J. Mpangile | Diwani Kata ya Ulembwe – Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya – **Mwenyekiti** |
| 2 | Ndg. Keneth A. Mgina | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji - **Katibu** |
| 3 | Mhe. Onesmo J. Lyandala | Diwani Kata ya Imalinyi – Makamu Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya |
| 4 | Mhe. Anaupendo E. Gombela | Diwani Kata ya Mdandu – Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji) - **Mjumbe** |
| 5 | Mhe. Fredrick E. Mwalongo | Diwani Kata ya Wangama - Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi na Mazingira- **Mjumbe** |
| 6 | Mhe. Happiness B. Bomber | Diwani Kata ya Udonja – Mwenyekiti Kamati ya Maadili ya Madiwani - **Mjumbe** |
| 7 | Mhe. Esteria E. Mbwilo | Diwani Viti maalum Tarafa ya Imalinyi – **Mjumbe** |
| 8 | Mhe. Wiston E. Mbilinyi | Diwani Kata ya Kidugala – **Mjumbe** |
| 9 | Mhe. Jane F. Kisakanike | Diwani Viti maalum Tarafa ya Wanging'ombe – **Mjumbe** |
| 10 | Mhe. Geofrey K. Nyagawa | Diwani Kata ya Wanging'ombe – **Mjumbe** |
| 11 | Mhe. Joseph R. Mjujulu | Diwani Kata ya Uhambule – **Mjumbe** |
| 12 | Mhe. Silvester J. Kigola | Diwani Kata ya Kijombe – **Mjumbe** |
| 13 | Mhe. Andrew G. Mangula | Diwani Kata ya Saja – **Mjumbe** |
| 14 | Mhe. Anthon E. Mahwata | Diwani Kata ya Igwachanya– **Mjumbe** |
| 15 | Mhe. Oliver H. Myale | Diwani Kata ya Ilembula - **Mjumbe** |
| 16 | Mhe. Damasco E. Mgaya | Diwani Kata ya Igosi – **Mjumbe** |
| 17 | Mhe. Mussa A. Sanga | Diwani Kata ya Kipengere – **Mjumbe** |
| 18 | Mhe. Magreth A. Kaduma | Diwani Viti maalum Tarafa ya Mdandu – **Mjumbe** |
| 19 | Mhe. Yustin L. Gudaga | Diwani Kata ya Usuka - **Mjumbe** |
| 20 | Mhe. Halfan R. Kawambwa | Diwani Kata ya Uhenga – **Mjumbe** |
| 21 | Mhe. Anna D. Madembwe | Diwani Viti maalumu Tarafa ya Imalinyi – **Mjumbe** |
| 22 | Mhe. Vumilia E. Kilamlya | Diwani Viti maalum Tarafa ya Mdandu – **Mjumbe** |
| 23 | Mhe. Paulina S. Mwinami | Diwani Kata ya Igima – **Mjumbe** |
| 24 | Mhe. Jelitha A. Fute | Diwani Viti maalum Tarafa ya Wanging'ombe – **Mjumbe** |
| 25 | Mhe. Victoria B. Mbiduka | Diwani Viti maalum Tarafa ya Imalinyi – **Mjumbe** |
| 26 | Mhe. Jairos L. Lunyungu | Diwani Kata ya Makoga - **Mjumbe** |
| 27 | Mhe. Thobias M. Mkane | Diwani Kata ya Itulahumba - **Mjumbe** |
| 28 | Mhe. Essau Th. Sanga | Diwani Kata ya Malangali – **Mjumbe** |

**WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA KWA TAARIFA**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Dkt. Festo J. Dugange | Naibu Waziri wa Nchi OR- TAMISEMI na Mbunge Jimbo la Wanging'ombe - **Mjumbe** |

**WAKUU WA IDARA/VITENGO WALIOHUDHURIA**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Odetha Banige | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Dkt. Frank Chiduo | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 3 | Ndg. Severine M. Mfuse | Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira |
| 4 | Ndg. Naili S. Mbyopyo | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 5 | Ndg. Joyce A. Mdemwa | Mratibu wa TASAF |
| 6 | Ndg. Happy Mkalawa | Afisa Ardhi |
| 7 | Ndg. Kasmiri David | Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki |
| 8 | Ndg. Omath Sanga | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 9 | Ndg. Ismail Lugemalila | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 10 | Ndg. Bernadeta C. Fivawo | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika |
| 11 | Ndg. Mohamed Ilunga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 12 | Ndg. Witness | Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 13 | Mhandisi Samson Mloge | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 14 | Ndg. Avit Rwehumbiza | Kny Mkuu wa Kitengo cha Mkaguzi wa Ndani |
| 15 | Dkt. Winson E. Mfikwa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi |
| 16 | Ndg. Rukia Mwelelwa | Katibu TSC |
| 17 | Ndg. Godfrey Banegura | Kny Afisa Ushirika |
| 18 | Ndg. Shimwe Manwingi | Kny Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 19 | Ndg. Anzawe J. Mgeni | Mhasibu |
| 20 | Ndg. Mulokozi A. Kishenyi | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 21 | Ndg. Demetrio K. Mgeni | Mthibiti Ubora wa Shule |
| 22 | Ndg. Rosemary Kapoma | Mratibu wa Mapambano Dhidi ya UKIMWI (CHAC) |
| 23 | Ndg. Christopher K. Masaaka | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |

**MAAFISA TARAFA WALIOHUDHURIA**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Emanuel I. Kingu | Afisa Tarafa – Tarafa ya Mdandu |
| 2 | Ndg. Damas Kavindi | Afisa Tarafa -Tarafa ya Wanging'ombe |
| 3 | Ndg. Hamza I. Zacharia | Afisa Tarafa – Tarafa ya Imalinyi |

**WAALIKWA WALIOHUDHURIA**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Lauteri J. Kanoni | Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe |
| 2 | Ndg. Edward N. Manga | Katibu Tawala Wilaya ya Wanging'ombe |
| 3 | Ndg. Anastazia Kibona | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi - Serikali za Mitaa Mkoa wa Njombe |
| 4 | Ndg. Silvia Mallya | Afisa Usalama Wilaya ya Wanging'ombe |
| 5 | SSP. Magnus Milinga | Mkuu wa Polisi Wilaya ya Wanging'ombe |
| 6 | Ndg. Scholastica Assey | Mkuu TAKUKURU Wilaya ya Wanging'ombe |
| 7 | Ndg. Dennis Nyambea | Afisa Uhamiaji Wilaya ya Wanging'ombe |
| 8 | Kadoda Komba | Mshauri wa Jeshi la Akiba Wilaya ya Wanging'ombe |
| 9 | S/SGT. Juma D. Muna | Afisa Magereza Wilaya ya Wanging'ombe |
| 10 | Ndg. Eliuteri Mworia | FMO |

**SEKRETARIETI**

| NA. | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Peter E. Chaula | Mwandishi wa Vikao |
| 2 | Ndg. Huruma O. Panja | Mwandishi wa Vikao |

**AJENDA ZA MKUTANO**

1. Kufungua mkutano.
2. Kupokea na kuridhia ajenda za mkutano.
3. Salamu za Serikali Kuu.
4. Taarifa ya Hesabu za mwaka (Final Accounts) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30, Juni 2021.
5. Kufunga mkutano.

**MUHTASARI NA. WDC/MMBM/14/09/2021/2022 – KUFUNGUA MKUTANO**

14:1 Katibu aliwasalimu wajumbe waliohudhuria mkutano huo.

14:2 Alimfahamisha Mwenyekiti kuwa, mkutano huo ni maalum kwa ajili ya kupitia taarifa ya Hesabu za Mwaka (Final Accounts) kwa mwaka fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021.

14:3 Alimtaarifu Mwenyekiti kuwa, Mkurugenzi Mtendaji yupo safari kikazi -Ofisi ya Rais TAMISEMI.

14:4 Aliwasilisha taarifa ya masikitiko ya kuungua kwa bweni katika Shule ya Sekondari Igima, alieleza kwamba, tukio hilo lilitokea tarehe 21.09.2021.

14:5 Baada ya taarifa hiyo, alimkaribisha Mwenyekiti afungue mkutano.

14:6 Kabla ya kufungua mkutano, Mwenyekiti alimkaribisha Makamu Mwenyekiti asome dua.

14:7 Makamu Mwenyekiti aliwaomba wajumbe waimbe wimbo wa Taifa na baada ya hapo, alisoma dua kwa ajili ya ufunguzi wa mkutano.

14:8 Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kuwa, mkutano huo ni muhimu kwa ajili ya kupitia taarifa ya Hesabu za Mwaka kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2021.

14:9 Aliwasihi wajumbe kupitia na kuijadili kwa kina taarifa hiyo, kwa maslahi ya Halmashauri.

14:10 Mwenyekiti alifungua mkutano saa **04:36** asubuhi.

**MUHTASARI NA. WDC/MMBM/15/09/2021/2022 – KUPOKEA AJENDA ZA MKUTANO**

15:1 Katibu alisoma ajenda tano zilizoandaliwa na kuziwasilisha kwa wajumbe.

15:2 Wajumbe walipokea na kuridhia ajenda zote tano kuwa, zijadiliwe kwenye mkutano huo.

**MUHTASARI NA. WDC/MMBM/16/09/2021/2022 – SALAMU ZA SERIKALI KUU**

16:1 Mwenyekiti alimkaribisha Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe awasalimu wajumbe na kuwasilisha Salamu za Serikali Kuu.

16:2 Mkuu wa Wilaya aliwasalimu wajumbe, wataalam na waalikwa waliohudhuria mkutano huo.

16:3 Aliwaeleza wajumbe kwamba, mkutano huo ni muhimu kwa ajili ya maandalizi ya ukaguzi wa nje (CAG) kwa mwaka 2020/2021, na kusisitiza kwamba, wajadili kwa umakini taarifa ya Hesabu za Mwaka (Final Accounts) kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 na kuweka hesabu vizuri ili kuwa na uhakika wa kuendelea kupata hati safi kwa ukaguzi ujao.

16:4 Aliwataarifu wajumbe kwa masikitiko kuhusu kuungua kwa bweni katika Shule ya Sekondari Igima, na kuagiza Jeshi la Polisi kuendelea kuwatafuta waliohusika na kuchoma bweni katika shule hiyo ili wafikishwe katika vyombo vya sheria.

16:5 Aliwafahamisha wajumbe kuwa, Serikali imetoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa mahindi katika Wilaya ya Wanging'ombe. Aidha, kupitia NFRA ununuzi wa mahindi umeshaanza katika kituo kilichopo Soko la Igula Kata ya Ilembula.

16:6 Ilielezwa kwamba, vikundi na AMCOS vinapewa kipaumbele kuuza mahindi NFRA.

16:7 Ilijulishwa kwa wajumbe kwamba, kwa sasa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imeagiza NFRA wanunue mahindi yote yaliyofikishwa katika kituo cha ununuzi wa mahindi Igula – Ilembula ili kuepuka malalamiko ya wananchi, baada ya hapo NFRA wataendelea na utaratibu uliowekwe.

16:8 Baada ya hapo, aliagiza yafuatayo:

i. Waheshimiwa Madiwani wawahamasishe wananchi kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO – 19. Wananchi waelimishwe kuwa, chanjo hiyo ni salama.

ii. Watendaji wa Kata wahamasishwe Wafanyabiashara wadogo kulipia kitambulisho cha ujasiriamali kwa njia ya mfumo. Watakaoshindwa kulipia kwa wakati Halmashauri ianze kuwatoza ushuru.

iii. Maandalizi yaendelee kufanyika ya mapokezi ya wanafunzi wa kuanza Kidato cha Kwanza kwa mwaka 2022, hususani

ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa na maabara.

iv. Waheshimiwa Madiwani na Wataalam wachangie mchango wa maafa ya kuungua kwa bweni katika Shule ya Sekondari Igima.

v. Halmashauri isaidie kununua magodoro na blanketi kwa ajili ya wanafunzi waliunguliwa bweni katika Shule ya Sekondari Igima.

vi. Waliohusika kutoa taarifa ambazo hazina usahihi kuhusu kuungua kwa bweni katika Shule ya Sekondari Igima, hususani kutoa idadi isiyosahihi ya wanafunzi waliokuwa wakiishi katika bweni lililoungua wachukuliwe hatua stahiki.

16:9 Mwenyekiti alishukuru kuwasilishwa kwa salamu za Serikali Kuu na kuwasilisha ombi kwamba, kiongezwe kituo kingine cha ununuzi wa mahindi hususani katika Tarafa ya Imalinyi iliyoko mbali na kituo kilichopo, ili kuwapunguzia gharama wakulima ya kusafirisha mahindi kupeleka soko la Igula – Ilembula.

16:10 Vile vile iliombwa, Mkuu wa Wilaya aliangalie kwa upana wake suala la NFRA kukata TZS.70 kwa kila kilo ya mahindi yanayouzwa na wakulima, kutokana na kiasi hicho kinachokatwa kuwa kikubwa na matumizi yake kutofahamika vizuri kwa wakulima.

16:11 Ilielezwa kwamba, wakulima wanalalamika kukatwa kiasi hicho.

16:12 Alisikitishwa kupokea taarifa ya kuungua kwa bweni katika Shule ya Sekondari Igima. Aliwaomba wajumbe kuchangi mchango wa kusaidia maafa ya kuungua kwa bweni katika shule hiyo.

**MUHTASARI NA. WDC/MMBM/17/09/2021/2022 – TAARIFA YA HESABU ZA MWAKA (FINAL ACCOUNTS) KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30, JUNI 2021**

17:1 Taarifa hiyo ilisomwa na kuwasilishwa kwa wajumbe.

17:2 Ilielezwa kwa wajumbe kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982, kifungu cha 40 pamoja na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa kifungu cha 31 ya mwaka 2010 kinazitaka Halmashauri zote nchini kuwa ziwe zinaandaa Hesabu za mwisho wa Mwaka na kuziwasilisha kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na kwa ajili ya ukaguzi ifikapo tarehe 30 Septemba ya Mwaka wa Fedha unaofuata.

17:3 Ilitaarifiwa kwa wajumbe kwamba, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, taarifa ya Hesabu za mwisho wa Mwaka zimeandaliwa kwa kuzingatia maeneo makuu manne ambayo ni:-

1. Taarifa ya mapato na matumizi (Financial Performance),
2. Mizania ya Hesabu (Financial Position),
3. Mtiririko wa Fedha (Cash Flow) na
4. Taarifa ya mabadiliko ya Mtaji (Statement of Changes in Net Asset).

17:4 **Kuhusu Mapato na Matumizi (Financial Performance)**

17:4:1 Ilifahamishwa kwa wajumbe kwamba, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Halmashauri ilikadiria kupokea na kukusanya Jumla ya **Shs. 28,380,360,016** na kufanikiwa kupokea kiasi cha **Tshs 24,668,746,227.96** kwa mchanganuo ufuatao:-

| **Chanzo** | **Makisio** | **Mapato Halisi** |
|---|---|---|
| Mishahara | 16,431,172,670.00 | 17,532,505,349.00 |
| Matumizi mengineyo | 1,308,220,000.00 | 1,231,625,104.28 |
| Miradi ya Maendeleo | 8,138,967,346.47 | 5,028,227,215.81 |
| Vyanzo vya ndani (own source) | 2,502,000,000.00 | 2,911,948,747.61 |
| **Jumla** | **28,380,360,016.00** | **24,668,746,227.96** |

17:4:2 **Kuhusu matumizi**, ilielezwa kwamba, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Halmashauri ilikadiria kutumia kiasi cha Tshs.**28,756,121,420.42** kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali ambazo mishahara, miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo.

17:4:3 Ilielezwa kwamba hadi kufikia tarehe 30, Juni, 2021 jumla ya Tshs **25,581,781,903.31** zilikuwa zimetumika kama ifuatavyo:-

| **Eneo la Matumizi** | **Makisio** | **Matumizi Halisi** |
|---|---|---|
| Mishahara | 16,431,172,670.00 | 17,271,196,647.00 |
| Matumizi mengineyo | 1,308,220,000.00 | 1,228,482,546.45 |
| Miradi ya maendeleo | 8,138,967,346.47 | 4,091,382,965.56 |
| Vyanzo vya ndani (own source) | 2,502,000,000.00 | 2,614,958,340.77 |
| Bakaa (Akaunti za Makao Makuu) | 375,761,403.53 | 375,761,403.53 |
| **Jumla** | **28,756,121,419.47** | **25,581,781,903.31** |

17:4:4 Ilifahamishwa kwa wajumbe kwamba, mapato na matumizi katika eneo la mishahara yanaonekana kuwa zaidi ya makisio kusudiwa kutokana na Serikali Kuu kulipa madeni ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi kwani katika mwaka wa fedha wa 2020/2021, Serikali imelipa kiasi cha Tshs. 902,011,546.71 kwa watumishi waliokuwa wakidai malimbikizo hayo.

17:5 **Mizania ya Hesabu (Financial Position)**

17:5:1 **Kuhusu thamani ya Mali**

17:5:1:1 Ilijulishwa kwa wajumbe kwamba, hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, ilikuwa na mali zenye thamani ya **Tshs. 39,682,782,647** ukilinganisha na **Tshs. 35,796,351,133** zilizokuwepo mwishoni mwa mwaka ulioishia 30 Juni 2020, na kuonekana kuwa zimeongezeka kutokana na kuongezeka kwa miundombinu ya ujenzi kama barabara na majengo, iliyotekelezwa katika mwaka 2020/2021 na ununuzi wa mali za kudumu ikiwemo magari, pikipiki na vifaa vya TEHAMA katika Halmashauri. Thamani ya mali ni baada ya kutoa kiasi cha uchakavu.

17:5:2 **Kuhusu madeni**

17:5:2:1 Ilitaarifiwa kwa wajumbe kwamba, hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021, Halmashauri ilikuwa na madeni halisi yenye thamani ya **Shs. 2,741,394,807** ambapo kati ya hayo, **Shs. 68,024,320** ni madeni ya Wazabuni waliotoa huduma kwa Halmashauri, na **Shs. 1,456,961,032** ni Madeni ya Watumishi. Pamoja na deni la **Tshs. 200,429,454.01** (Mfuko wa Wanawake na Vijana Shs. 67,091,071.44, asilimia mbili ya wakusanyaji za mwezi Aprili, 2021 Shs. 5,139,084 na asilimia 20 ya makusanyo ya miezi ya Mei na Juni, 2021 TZS. 128,199,298.57) ambazo hazikupelekwa katika Mifuko husika kutokana na ukomo wa bajeti ya mwaka 2020/2021 na salio la mfuko wa amana **Shs. 429,916,649.41** ukilinganisha na madeni ya kiasi cha Shs. **3,153,291,426** ya mwaka wa fedha wa 2019/2020.

17:5:2:2 Ilielezwa kwamba, mchanganuo wa madeni ya watumishi ni kama ilivyoainishwa katika jedwali lifuatalo

| | **Likizo** | **Matibabu** | **Mafunzo** | **Uhamisho** | **Posho za Kujikimu** | **Malimbikizo ya mishahara** | **Madai mengineyo** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Madeni ya walimu | - | 2,672,000 | 2,805,600 | 152,896,610 | 1,767,000 | 103,933,600 | 43,078,000 | 307,152,810 |
| Madeni ya wasio walimu | 3,722,980 | - | - | 73,501,430 | 119,586,437 | 510,469,348 | 442,528,027 | 1,149,808,222 |
| **Jumla** | **3,722,980** | **2,672,000** | **2,805,600** | **226,398,040** | **121,353,437** | **614,402,948** | **485,606,027** | **1,456,961,032** |

17:6 **Kuhusu Mtiririko ya Fedha (Cash Flow)**

17:6:1 Ilielezwa kwamba, taarifa hii inaonesha mtiririko wa fedha baada ya kulinganisha na kuondoa gharama na mapato ambayo hayajumuishi fedha taslimu au halisi (mfano uchakavu). Aidha, taarifa hii, imegawanyika katika vipengele vikuu vitatu ambavyo ni:

i. Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kawaida (Operating Activities)
ii. Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji (Investing Activities)
iii. Mtiririko wa fedha kutokana na mitaji katika uwekezaji (Financing Activities)

17:6:2 Ilifafanuliwa kwamba, mtiririko wa mapato kutokana na shughuli za kawaida unaonesha kwamba kiasi cha **Tshs. 24,333,250,516** zilikuwa zimekusanywa na kiasi cha **Tshs. 23,550,047,300** zilikuwa zimetumika na hivyo Halmashauri kuwa imetumia pungufu kwa kiasi cha **Sh. 783,203,217.** Kiasi cha matumizi kinajumuisha mali ghalani (inventory) za mwaka uliopita ambazo zimetumika katika mwaka wa fedha wa taarifa hii pamoja na salio katika akaunti za Halmashauri kwa mwaka uliopita.

17:7 **Kuhusu mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji (Investing Activities)**

17:7:1 Ilielezwa kwamba, kutokana na shughuli za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe ilitumia kiasi cha **Shs.3,602,640,940** kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa mali za kudumu, ujenzi wa miundo mbinu pamoja na rasilimali mbalimbali za Halmashauri ikilinganishwa na matumizi ya Miradi kwa Mwaka 2019/2020 ambapo jumla ya **Sh.2,625,670,508** zilikuwa zimetumika.

17:8 **Kuhusu mtiririko wa fedha kutokana na mitaji katika uwekezaji (Financing Activities)**

17:8:1 Ilifahamishwa kwa wajumbe kwamba, katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30, Juni 2021, jumla ya **Shs 4,254,723,076** zilielekezwa kugharamia ununuzi wa mali za kudumu, ikilinganishwa na mwaka wa fedha wa 2019/2020 ambapo **Shs 2,029,008,919** zilitumika.

17:9 **Kuhusu Salio la Fedha katika Akaunti za Halmashauri (Cash and Cash Equivalent)**

17:9:1 Ilifafanuliwa kwa wajumbe kwamba, hadi kufikia tarehe 30.06.2021 Halmashauri ilikuwa imebaki na jumla ya **Sh. 3,471,299,623** katika taarifa ya Hesabu za mwisho wa Mwaka, kati ya hizo, jumla ya **Sh. 1,564,345,703** ilikuwa ni fedha zilizosalia kwenye Akaunti za Halmashauri (Makao Makuu), na **Sh. 1,906,953,919** zilikuwa zimebaki kwenye Akaunti za Shule, Kata na Zahanati kwa mchanganuo ufuato:

| Na | Jina la Akaunti | Kiasi (Salio) |
|---|---|---|
| 1 | Mfuko wa Maendeleo | 826,731,498 |
| 2 | Mfuko wa Matumizi Mengineyo (GF) | 226,440,334 |
| 3 | Mfuko wa Mapato ya Ndani | 20,362,308 |
| 4 | Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu | 60,894,914 |
| 5 | Mfuko wa Amana | 429,916,649 |
| **Jumla Ndogo – Salio la Akaunti za Halmashauri** | | **1,564,345,703** |
| 6 | Akaunti za Kata | 105,042,250 |
| 7 | Akaunti za Shule za Msingi | 550,277,740 |
| 8 | Akaunti za Shule za Sekondari | 628,141,397 |
| 9 | Akaunti za Vituo vya Afya na Zahanati | 623,492,531 |
| **Jumla Ndogo – Salio la Akaunti za Shule, Kata na Vituo vya Afya** | | **1,906,953,919** |
| **Jumla Kuu** | | **3,471,299,623** |

17:9:2 Ilielezwa kwamba, mchanganuo wa fedha katika akaunti za miradi ya maendeleo ni kama ifuatavyo:

| Na | Mradi | Kiasi (Salio) - Tsh |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Mfuko wa WYDF | 66,856,545.06 |
| 2 | Fedha za miradi ya kimkakati | 62,266,865.06 |
| 3 | Mpango wa kunusuru Kaya maskini | 5,421,351.76 |
| 4 | Asilimia 20 ya LLG | 124,494,541.08 |
| 5 | Fedha za ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri | 67,593,401.25 |

17:9:3 Mchanganuo wa salio la fedha katika Mfuko wa Amana ni kama ilivyoainishwa hapa chini;

i. Fedha za zuio (Retention) Tshs. 334,773,715.50.
ii. Mfuko wa Global Funds Tshs. 29,996.82.
iii. Salio la fedha za uendeshaji wa mitihani ya darasa la saba Tshs. 72,717,339.26.
iv. Amana nyingine Tshs. 22,395,597.83

17:9:4 Ilielezwa kwamba, salio la fedha katika akaunti za shule za msingi, sekondari na vituo vya kutolea huduma za afya ni kubwa kutokana na fedha za miradi ya ujenzi kupokelewa mwishoni mwa mwaka wa fedha (ambapo shule za msingi na sekondari zilipokea Tsh. 1,000,000,000.00 kwa ajili ya miradi ya ujenzi na Zahanati ya Saja ilipokea kiasi cha Tsh. 500,000,000.00)

17:10 **Kuhusu Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji (Statement of Changes in Net Asset)**

17:10:1 Ilitaarifiwa kwa wajumbe kwamba, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, mtaji uliongezeka mpaka kufikia kiasi cha **Sh. 3,362,550,621** ikilinganishwa na **Sh. 485,284,972** za Mwaka wa Fedha 2019/2020.

17:11 **Kuhusu Uwezo wa Halmashauri**

17:11:1 Ilielezwa kwamba, taarifa hii inaonesha kuwa, Halmashauri inao uwezo wa kulipa madeni yake (current liability) kwa kulinganisha mali (current assets) na madeni. Ingawa Halmashauri inategemea kwa kiasi kikubwa ruzuku ya Serikali ambapo makusanyo yanayotokana na vyanzo vya ndani ni sawa na asilimia **9%** ya makusanyo yote.

17:12 Wajumbe walipokea taarifa ya Hesabu za mwaka (Final Accounts) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30, Juni 2021 na kuipitia ukurasa kwa ukurasa pamoja na viambatanisho vyake.

17:13 Wajumbe waliipongeza Menejimenti, kwa kuandaa taarifa nzuri ya Hesabu za mwaka (Final Accounts) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30, Juni 2021. Vile vile walishukuru kwa uwasilishaji makini wa taarifa hiyo.

17:14 Kuhusu madeni, ilishauriwa yaandikwe kwa kuzingatia uhalisia kutokana na baadhi ya madeni kulipwa.

17:15 Wajumbe waliridhia na kupitisha taarifa ya Hesabu za mwaka (Final Accounts) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30, Juni 2021 za

Halmashauri, iwasilishwe Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Ofisi ya Mkaguzi wa Nje Mkoa (CEA).

**MUHTASARI NA. WDC/MMBM/18/09/2021/2022 – KUFUNGA MKUTANO**

18:1 Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge mkutano.

18:2 Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kupitia na kupitisha taarifa ya Hesabu za Mwaka (Final Accounts) kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2021.

18:3 Alimshukuru Mkuu wa Wilaya, wajumbe waalikwa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya (Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya) na Mkoa (Katibu Tawala Msaidizi Mkoa/Afisa Serikali za Mitaa Mkao) kwa kushiriki mkutano huo.

18:4 Mwenyekiti alifunga mkutano saa **05:23** asubuhi.

**NAIDHINISHA UPELEKWE/USAMBAZWE KWA WAJUMBE**

..........................................

Maryam A. Muhaji

**Katibu**

Tarehe...22/10/2021...

***UMETHIBITISHWA***

| | |
|---|---|
| ........................................... | ..................................... |
| Ndg. Keneth A. Mgina | Agnetha J. Mpangile |
| **Katibu** | **Mwenyekiti** |
| Tarehe............................ | Tarehe......................... |

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

# TAARIFA YA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE KWENYE MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 28-29/10/2021

# YALIYOMO


| NA | JINA LA KAMATI | UKURASA |
|---|---|---|
| 1 | Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango | 1 - 8 |
| 2 | Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi Ardhi, Maliasili na Mazingira | 9 - 11 |
| 3 | Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji) | 12 - 14 |

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

*Kwenda kwa*: Mheshimiwa Mwenyekiti,
**Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe**

*Kutoka kwa*: Wenyeviti wa Kamati za Kudumu,
**Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe**

**TAARIFA YA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE KWENYE MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 28-29/10/2021**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Kamati za Kudumu za Halmashauri ya Wilaya zimefanya vikao kwa kipindi cha kuanzia mwezi Juni hadi Septemba, 2021 robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ilivyopangwa kufanyika kwa kila kikao cha Kamati husika. Kamati zinazowasilisha taarifa hizo ni pamoja na:-

i. Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango,
ii. Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi, Maliasili na Mazingira na
iii. Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji).

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kila kamati tajwa hapo juu, imetekeleza shughuli mbalimbali kwa kipindi husika kama ilivyoainishwa hapa chini:

## A) KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO

**I Kikao cha kawaida cha tarehe 30.07.2021**

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA WAKE |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Agnetha J. Mpangile | Diwani Kata ya Ulembwe – Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya – **Mwenyekiti** |
| 2 | Ndg. Edes P. Lukoa | Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya -**Katibu** |
| 3 | Mhe. Onesmo J. Lyandala | Diwani Kata ya Imalinyi – Makamu Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya |
| 4 | Mhe. Fredrick E. Mwalongo | Diwani Kata ya Wangama – Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi, Maliasili na Mazingira - **Mjumbe** |
| 5 | Mhe. Anaupendo E. Gombela | Diwani Kata ya Mdandu – Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji) - **Mjumbe** |
| 6 | Mhe. Esteria E. Mbwilo | Diwani Viti maalum Tarafa ya Mdandu – **Mjumbe** |

WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA WAKE |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Dkt Festo John Dugange | Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe - **Mjumbe** |

WAKUU WA IDARA/VITENGO WALIOHUDHURIA

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Odetha Banige | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala |
| 2 | Ndg. Omath Sanga | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari. |
| 3 | Ndg. Fredrick Sigachuma | Kny Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. |
| 4 | Ndg. Rukia Mwelelwa | Katibu TSC. |
| 5 | Ndg. Demetrio Mgeni | Mthibiti Ubora wa shule. |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Ndg. Severine Mfuse | Kny Mkuu wa Kitengo cha Nyuki. |
| 8 | Ndg. Carystus Kihaka | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi. |
| 9 | Eng. Samson Mloge | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi. |
| 11 | Ndg. Rosemary Kapoma | Mratibu wa UKIMWI (CHAC). |
| 12 | Ndg. Mulokozi Kishenyi | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara. |
| 13 | Ndg. Omega Kagine | Kny Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi. |
| 14 | Ndg. Richard Msigwa | Kny Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika. |
| 15 | Ndg. Rosemary Msorolo | Kny Afisa Biashara. |
| 16 | Ndg. Ismail Lugemalila | Kny Mkuu wa Kitengo cha Mkaguzi wa Ndani. |
| 17 | Ndg. Mathias Lyabonga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 18 | Ndg. Naili S. Mbyopyo | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 19 | Ndg. Amon P. Chalamila | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA. |
| 20 | Ndg. Frank Ngogo | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Mazingira. |
| 22 | Dr. Frank Chiduo | Mganga Mkuu wa Wilaya |
| 23 | Ndg. Godfrey Benegula | Kny Afisa Ushirika |
| 24 | Ndg. Telesphory Myamba | Afisa Biashara |

**MAAFISA TARAFA**

| NA | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Damas Kavindi | Afisa Tarafa – Wanging'ombe |
| 2 | Ndg. Hamza Zacharia | Afisa Tarafa - Imalinyi |
| 3 | Ndg. Emanuel Kingu | Afisa Tarafa -Mdandu |

**MAAFISA TARAFA WALIOHUDHURIA**

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Emanuel J. Kingu | Afisa Tarafa – Tarafa ya Mdandu |
| 2 | Ndg. Hamza I. Zacharia | Afisa Tarafa – Tarafa ya Imalinyi |
| 3 | Ndg. Damas Kavindi | Afisa Tarafa – Tarafa ya Wanging'ombe |

**SEKRETARIETI**

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Huruma O. Panja | Mwandishi wa Vikao |
| 2 | Ndg. Peter E. Chaula | Mwandishi wa Vikao |

**AJENDA ZA KIKAO**

1. Kufungua kikao.
2. Kupokea ajenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao maalum cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 02.06.2021.
4. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 17.06.2021
5. Kusoma na kujadili utekelezaji wa maazimio ya kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 17.06.2021.
6. Taarifa, maombi na mapendekezo Mbalimbali:-
   i. Mapato na Matumizi ya mwezi Juni, 2021.
   ii. Ukaguzi wa ndani uliofanywa na Mkaguzi wa Ndani kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021.
   iii. Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021..
   iv. Utawala na utumishi.
   v. Manunuzi yaliyofanyika kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021.
   vi. Kesi mbalimbali za Halmashauri.

vii. Kusitishwa kwa matumizi ya Mfumo wa malipo wa EPICOR na kuanza kutumia mfumo wa MUSE.
viii. Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na mapendekezo.
ix. Rasimu ya Sheria Ndogo ya Uanzishwaji wa Mfuko wa Elimu 2021 katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.
x. Maombi ya kiasi cha TZs.58,555,000.00 katika Mfumo wa Amana.
xi. Maombi ya TZs.36,400,000.00 kwa ajili ya posho ya waajiriwa wapya 96.
xii. Mapendekezo ya gharama za uchangiaji kwenye vituo vya huduma za afya kuanzia Julai Mosi 2021.
xiii. Mapendekezo ya usimamizi na uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii (i-CHF) iliyoboreshwa.
xiv. Mapendekezo ya ratiba ya vikao kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
xv. Mapokezi ya Gari STL. 9378.
xvi. Ombi la ofisi kwa Taasisi
xvii. Ununuzi wa Gari aina ya Suzuki Jimny SM.13781.
viii. Mapendekezo ya matumizi ya fedha shs. 2,875,445,810.13 zilizovuka (bakaa) mwaka toka mwaka 2020/21 kwenda mwaka 2021/22.
ix. Matokeo ya zabuni ya nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji.
x. Mpango kazi wa Mkaguzi wa Ndani kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
xi. Mapendekezo ya kuanzisha kiwanda cha tofali.
xii. Masula ya Kiutumishi.

7. Kufunga kikao.

**UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 30.07.2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI**

| NA | AZIMIO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | **MUHTASARI NA. WDC/KFUM/05/07/2021/2022**<br>Dondoo Na. 5:3:2:3<br><br>**AZIMIO:**Kikao kijacho uwasilishwe mchanganuo wa watumishi wa Idara ya Afya watakaohamishiwa katika Zahanati ya Idunda, Idindilimunyu, Gonelamafuta, Mafinga, Itambo na Mawindi anayehamishwa atalipwa shilingi ngapi na vigezo/sababu za kutofautiana kwa malipo hayo. | Azimio limezingatiwa, angalia *Kiambatisho* **"A"** |
| 2 | **MUHTASARI NA. WDC/KFUM/06/07/2021/2022**<br>Dondoo Na. 7:2:4:3:5<br><br>**AZIMIO:**Kikao kijacho iwasilishwe taarifa ya hoja ya Marehemu Gervas Kadodo ya kulipwa mshahara wakati hayuko kazini ikiwa imefungwa. | Azimio limetekelezwa, kiasi cha Tshs.793,603.44 kilishalipwa tayari. |
| 3 | **MUHTASARI NA. WDC/KFUM/06/07/2021/2022**<br>Dondoo Na. 7:2:4:6:3<br><br>**AZIMIO:**Kikao kijacho iwasilishwe taarifa hoja ya malipo yaliyofanyika bila hati ya malipo ya TZS.15,827,728 katika shule ya Msingi Igwachanya na Hati za malipo zilizokosekana za TZS.3,261,411.00 katika shule ya Msingi Igwachanya. | Azimio limetekelezwa nyaraka zilishawasilishwa kwa Mkaguzi wa Ndani na hoja hiyo imefungwa. |
| 4 | **MUHTASARI NA. WDC/KFUM/06/07/2021/2022**<br>Dondoo Na. 7:18:4:4 | Azimio limezingatiwa, kikao kilishafanyika tarehe tarehe **03.08.2021** siku ya Jumanne |

| | | |
|---|---|---|
| | **AZIMIO:** Kiitishwe kikao maalum kwa ajili ya kujadili taarifa ya matokeo ya zabuni ya nyumba ya Mkurugenzi na Marejeo ya bajeti ya mwaka wa fedha, 2021/2022. | katika ukumbi wa Halmashauri. |

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe **30.07.2021**, wajumbe wa kamati hii, walipitisha taarifa, maombi na mapendekezo mbalimbali kama ilivyoainishwa hapa chini:-

i. Mapato na Matumizi ya mwezi Juni, 2021.
ii. Ukaguzi wa ndani uliofanywa na Mkaguzi wa Ndani kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021.
iii. Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021.
iv. Utawala na utumishi.
v. Manunuzi yaliyofanyika kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021.
vi. Kesi mbalimbali za Halmashauri.
vii. Kusitishwa kwa matumizi ya Mfumo wa malipo wa EPICOR na kuanza kutumia mfumo wa MUSE.
viii. Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na mapendekezo.
ix. Rasimu ya Sheria Ndogo ya Uanzishwaji wa Mfuko wa Elimu 2021 katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.
x. Maombi ya kiasi cha TZs.58,555,000.00 katika Mfumo wa Amana.
xi. Maombi ya TZs.36,400,000.00 kwa ajili ya posho ya waajirirwa wapya 96.
xii. Mapendekezo ya gharama za uchangiaji kwenye vituo vya huduma za afya kuanzia Julai Mosi 2021.
xiii. Mapendekezo ya usimamizi na uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii (i-CHF) iliyoboreshwa.
xiv. Mapendekezo ya ratiba ya vikao kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
xv. Mapokezi ya Gari STL. 9378.
xvi. Ombi la ofisi kwa Taasisi.
xvii. Ununuzi wa Gari aina ya Suzuki Jimny SM.13781.
xviii. Mapendekezo ya matumizi ya fedha shs. 2,875,445,810.13 zilizovuka (bakaa) mwaka toka mwaka 2020/21 kwenda mwaka 2021/22.
xix. Matokeo ya zabuni ya nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji.
xx. Mpango kazi wa Mkaguzi wa Ndani kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
xxi. Mapendekezo ya kuanzisha kiwanda cha tofali.
xxii. Masula ya Kiutumishi.

**II Kikao cha kawaida cha tarehe 19.08.2021**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA WAKE |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Agnetha J. Mpangile | Diwani Kata ya Ulembwe – Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya – **Mwenyekiti** |
| 2 | Ndg. Ferd Y. Mhanze | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya **-Katibu** |
| 3 | Mhe. Onesmo J. Lyandala | Diwani Kata ya Imalinyi – Makamu Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya |
| 4 | Mhe. Fredrick E. Mwalongo | Diwani Kata ya Wangama – Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi, Maliasili na Mazingira - **Mjumbe** |
| 5 | Mhe. Anaupendo E. Gombela | Diwani Kata ya Mdandu – Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji) - **Mjumbe** |
| 6 | Mhe. Esteria E. Mbwilo | Diwani Viti maalum Tarafa ya Imalinyi – **Mjumbe** |

WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA WAKE |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Dkt Festo John Dugange | Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe - **Mjumbe** |

WAKUU WA IDARA/VITENGO WALIOHUDHURIA

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Odetha Banige | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala |
| 2 | Ndg. Omath Sanga | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari. |
| 3 | Ndg. Winson Mfikwa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. |
| 4 | Ndg. Rukia Mwelelwa | Katibu TSC. |
| 5 | Ndg. Demetrio Mgeni | Mthibiti Ubora wa shule. |
| 6 | Ndg. Kasmir David | Mkuu wa Kitengo cha Nyuki. |
| 7 | Ndg. Juma Chalamila | Kny Afisa Uchaguzi |
| 8 | Ndg. Carystus Kihaka | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi. |
| 9 | Eng. Samson Mloge | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi. |
| 12 | Ndg. Mulokozi Kishenyi | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara. |
| 13 | Ndg. Fadhili Msilu | Kny Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi. |
| 14 | Ndg. Richard Msigwa | Kny Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika. |
| 15 | Ndg. Rosemary Msorolo | Mhasibu wa Mapato |
| 16 | Ndg. Ismail Lugemalila | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mkaguzi wa Ndani. |
| 17 | Ndg. Mathias Lyabonga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 18 | Ndg. Naili S. Mbyopyo | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 19 | Ndg. Amon P. Chalamila | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA. |
| 20 | Ndg. Frank Ngogo | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Mazingira. |
| 21 | Ndg. Cosmas Bujah | Afisa Ardhi |
| 22 | Dr. Frank Chiduo | Mganga Mkuu wa Wilaya |
| 23 | Ndg. Fredrick Sigachuma | Kny Afisa Ushirika |
| 24 | Ndg. Yusta Mwambembe | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 25 | Ndg. Keneth Mgina | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 26 | Ndg. Telesphory Myamba | Afisa Biashara |

MAAFISA TARAFA

| NA | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Harid Kapela | Kny Afisa Tarafa – Wanging'ombe |
| 2 | Ndg.Bathromeo Mgaya | Kny Afisa Tarafa - Imalinyi |
| 3 | Ndg. Yohana B. Haule | Kny Afisa Tarafa -Mdandu |

SEKRETARIETI

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Huruma O. Panja | Mwandishi wa Vikao |
| 2 | Ndg. Peter E. Chaula | Mwandishi wa Vikao |

AJENDA ZA KIKAO

1. Kufungua kikao.
2. Kupokea ajenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 30.07.2021.
4. Kusoma na kujadili utekelezaji wa maazimio ya kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 30.07.2021.
5. Taarifa, maombi na mapendekezo Mbalimbali:-
    i. Mapato na Matumizi ya mwezi Julai, 2021.
    ii. Miradi ya maendeleo itakayoombewa fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

iii. Mapokezi ya fedha kiasi cha TZS.39,600,000.00 za ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule za msingi.
iv. Maombi ya mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu vinavyopendekezwa kupewa mikopo kwa kipindi cha robo ya kwanza mwaka, 2021/2022.
v. Maombi ya fedha kiasi cha TZS.72,717,339.26 ambazo ni bakaa ya Idara ya Elimu Msingi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya malipo ya madai mbalimbali ya watumishi pamoja na uendeshaji wa Mitihani ya Mock darasa la IV 2021.
vi. Mapendekezo ya miradi itakayopelekewa fedha ya mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi ya maendeleo.
vii. Mapendekezo ya kubadili watia saini wa Akaunti za Halmashauri na Vituo vya kutolea huduma za Afya na Elimu.

6. Kufunga kikao.

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** katika kikao cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe **19.08.2021**, wajumbe wa kamati hii, walipitisha taarifa, maombi na mapendekezo mbalimbali kama ilivyoainishwa hapa chini:-

i. Mapato na Matumizi ya mwezi Julai, 2021.
ii. Miradi ya maendeleo itakayoombewa fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
iii. Mapokezi ya fedha kiasi cha TZS.39,600,000.00 za ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule za msingi.
iv. Maombi ya mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu vinavyopendekezwa kupewa mikopo kwa kipindi cha robo ya kwanza mwaka, 2021/2022.
v. Maombi ya fedha kiasi cha TZS.72,717,339.26 ambazo ni bakaa ya Idara ya Elimu Msingi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya malipo ya madai mbalimbali ya watumishi pamoja na uendeshaji wa Mitihani ya Mock darasa la IV 2021.
vi. Mapendekezo ya miradi itakayopelekewa fedha ya mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi ya maendeleo.
vii. Mapendekezo ya kubadili watia saini wa Akaunti za Halmashauri na Vituo vya kutolea huduma za Afya na Elimu.

**III Kikao cha kawaida cha tarehe 15.09.2021**

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA WAKE |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Agnetha J. Mpangile | Diwani Kata ya Ulembwe-Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya- **Mwenyekiti** |
| 2 | Ndg. Maryam A. Mhaji | Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya- **Katibu** |
| 3 | Mhe. Onesmo J. Lyandala | Diwani Kata ya Imalinyi- Makamu Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya- **Mjumbe** |
| 4 | Mhe. Fredrick E. Mwalongo | Diwani Kata ya Wangama –Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi, Maliasili na Mazingira-**Mjumbe** |
| 5 | Mhe. Anaupendo E. Gombela | Diwani Kata ya Mdandu-Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji) **–Mjumbe** |
| 6 | Mhe. Esteria E. Mbwilo | Diwani Viti Maalum Tarafa ya Imalinyi **-Mjumbe** |

WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA WAKE |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Dkt Festo J. Dugange | Mbunge Jimbo la Wanging'ombe- Mjumbe |

WAKUU WA IDARA/VITENGO WALIOHUDHURIA

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Odetha Banige | Kaimu Mkuu Idara ya Utumishi na Utawala |
| 2 | Ndg. Omath Sanga | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 3 | Ndg. Winson Mfikwa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Mifuugo na Uvuvi |
| 4 | Ndg. Rukia Mwelelwa | Katibu TSC |
| 5 | Ndg. Demetrio Mgeni | Mthibiti Ubora wa shule |
| 6 | Ndg. Kasmiri David | Mkuu wa Kitengo cha Nyuki |
| 7 | Ndg. Juma Chalamila | Kny. Afisa Uchaguzi |
| 8 | Ndg. Carystus Kihaka | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 9 | Ndg. Samson Mloge | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 10 | Ndg. Mulokozi Kishenyi | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 11 | Ndg. Mohamed Ilunga | Kny. Mkuu wa idara ya Elimu Msingi |
| 12 | Ndg. Bernadeta Fivawo | Mkuu wa Idara ya kilimo, Umwagiliaji na Ushirika |
| 13 | Ndg. Rosemary Msorolo | Mhasibu wa Mapato |
| 14 | Ndg. Ismail Lugemalila | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mkaguzi wa Ndani |
| 15 | Ndg. Mathias Lyabonga | Kaimu Mkuu Idara ya Mipango, Takwimu na Ufwatiliaji |
| 16 | Ndg. Naili S. Mbyopyo | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 17 | Ndg. Amon P. Chalamila | Kaimu Mkuu Kitengo cha TEHAMA |
| 18 | Ndg. Severine Mfuse | Kny. Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Mazingira |
| 19 | Ndg. Cosmas Bujah | Afisa Ardhi |
| 20 | Ndg. Boniface Msemwa | Kny. Mganga Mkuu wa Wilaya |
| 21 | Ndg. Felician Shantiwa | Afisa Ushirika |
| 22 | Ndg. Onolasco Mwogofi | Kny. Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 23 | Ndg. Telesphory Myamba | Afisa Biashara |

MAAFISA TARAFA

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Hamza Zacharia | Afisa Tarafa – Imalinyi |
| 2 | Ndg. Damas Kavindi | Afisa Tarafa - Wanging'ombe |
| 3 | Ndg. Emanuel Kingu | Afisa Tarafa - Mdandu |

SEKRETARIETI

| NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Huruma Panja | Mwandishi wa Vikao |
| 2 | Ndg. Peter E. Chaula | Mwandishi wa Vikao |

AJENDA ZA KIKAO

1. Kufungua Kikao.
2. Kupokea ajenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 19.08.2021.
4. Taarifa, maombi na mapendekezo mbalimbali:-
    i. Mapato na Matumizi ya mwezi Agostii, 2021.
    ii. Taarifa ya mpango wa mafunzo kwa watumishi wanaotakiwa kwenda masomoni na waliopo masomoni kwa mwaka wa fedha, 2021/2022.
    iii. Taarifa ya marejesho ya mikopo ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na wenye Ulemavu kwa mwezi Agosti, 2021.
    iv. Taarifa ya utekelezajiwa wa shughuli za Kitengo cha TASAF.
    v. Mpango wa manunuzi kwa mwaka wa fedha, 2021.
    vi. Ombi la fedha za kukamilisha majengo ya Hospitali ya Wilaya.

vii. Ombi la kubadili matumizi ya fedha TZS.13,000,000.00 iliyotakiwa kutumika kwenye maonesho ya nanenane 2021 ili itumike kwenye maandalizi ya kitalu cha Parachichi cha Halmashauri.

viii. Mapendekezo ya ujenzie wa Kituo cha Afya katika Tarafa ya Mdandu.

ix. Mapendekezo ya ugawaji wa pikipiki watakazonunuliwa watumishi wa kilimo na mifugo kwa mwaka wa fedha, 2021,2022.

x. Mapendekezo ya miradi itakayopelekewa fedha kutoka mapato ya ndani ya mwezi Agosti, 2021.

xi. Kuwasilisha taarifa ya tathimini ya miradi ya kuomba fedha.

5. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.
6. Kufunga kikao.

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kikao cha tarehe **15.09.2021**, wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango walipitisha taarifa, maombi ya fedha na mapendekezo mbalimbali kama ilivyoainshwa hapa chini:

i. Mapato na Matumizi ya mwezi Agostii, 2021.

ii. Taarifa ya mpango wa mafunzo kwa watumishi wanaotakiwa kwenda masomoni na waliopo masomoni kwa mwaka wa fedha, 2021/2022.

iii. Taarifa ya marejesho ya mikopo ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na wenye Ulemavu kwa mwezi Agosti, 2021.

iv. Taarifa ya utekelezajiwa wa shughuli za Kitengo cha TASAF.

v. Mpango wa manunuzi kwa mwaka wa fedha, 2021.

vi. Ombi la fedha za kukamilisha majengo ya Hospitali ya Wilaya.

vii. Ombi la kubadili matumizi ya fedha TZS.13,000,000.00 iliyotakiwa kutumika kwenye maonesho ya nanenane 2021 ili itumike kwenye maandalizi ya kitalu cha Parachichi cha Halmashauri.

viii. Mapendekezo ya ujenzie wa Kituo cha Afya katika Tarafa ya Mdandu.

ix. Mapendekezo ya ugawaji wa pikipiki watakazonunuliwa watumishi wa kilimo na mifugo kwa mwaka wa fedha, 2021,2022.

x. Mapendekezo ya miradi itakayopelekewa fedha kutoka mapato ya ndani ya mwezi Agosti, 2021.

xi. Kuwasilisha taarifa ya tathimini ya miradi ya kuomba fedha.

**UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREH 15.09.2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI**

| NA | AZIMIO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1. | **MUHTASARI NA. WDC/KFUM/26/08/2021/2022**<br>Dondoo Na.24:1:8:10<br><br>**AZIMIO:**Kikao kijacho iwasilishwe taarifa ya kiasi gani cha asilimia kimepelekwa Katani kuanzia mwezi Aprili hadi Agosti, 2021. | Azimio limezingatiwa, angalia kiambatisho **"A"** |

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, ninaomba kuwasilisha.

.............................

Mhe. Agnetha J. Mpangile

**Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango**

B) KAMATI YA HUDUMA ZA UCHUMI, UJENZI, ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA

**I Kikao cha kawaida cha tarehe 24.07.2021**

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| NA | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Mhe.Fredrick E. Mwalongo | Diwani Kata ya Wangama – **Mwenyekiti** |
| 2 | Ndg. Bernadeta Fivawo | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji - **Katibu** |
| 3 | Mhe.Agnetha J. Mpangile | Diwani Kata ya Ulembwe – Mwenyekiti wa Halmashauri |
| 4 | Mhe.Unesmo J.Lyandala | Diwani Kata ya Imalinyi – Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri |
| 5 | Mhe.Paulina S. Mwinami | Diwani Kata ya Igima – **Mjumbe** |
| 6 | Mhe.Jairos L. Lunyungu | Diwani Kata ya Makoga - **Mjumbe** |
| 7 | Mhe.Victoria B. Mbiduka | Diwani Viti maalumu Tarafa ya Imalinyi – **Mjumbe** |
| 8 | Mhe.Andrew G. Mangula | Diwani Kata ya Saja – **Mjumbe** |
| 9 | Mhe.Happiness B. Bomber | Diwani Kata ya Udonja – **Mjumbe** |
| 10 | Mhe.Anna D. Madembwe | Diwani Viti maalumu Tarafa ya Imalinyi - **Mjumbe** |
| 11 | Mhe.Jane F. Kisakanike | Diwani Viti maalumu Tarafa ya Wanging'ombe – **Mjumbe** |
| 12 | Mhe.Damasco E. Mgaya | Diwani Kata ya Igosi – **Mjumbe** |
| 13 | Mhe.Geofrey K. Nyagawa | Diwani Kata ya Wanging'ombe – **Mjumbe** |
| 14 | Mhe.Joseph R. Mjujulu | Diwani Kata ya Uhambule – **Mjumbe** |
| 15 | Mhe.Anthon E. Mahwata | Diwani Kata ya Igwachanya – **Mjumbe** |

WAKUU WA IDARA/VITENGO WALIOHUDHURIA

| NA | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg.Odetha Banige | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |
| 2 | Ndg.Yusufu Yahaya | Kny Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 3 | Ndg.Amon P. Chalamila | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 4 | Ndg.Albert Mwakipesile | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 5 | Ndg.Frank Ngogo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira |
| 6 | Ndg.Severine Mfuse | Kny Mkuu wa Kitengo cha Ufungaji Nyuki |
| 7 | Ndg.Mohamed Ilunga | Kny Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 8 | Ndg.Rukia Mwelelwa | Katibu TSC |
| 9 | Ndg.Visia Chapile | Mratibu wa Mapambano Dhidi ya UKIMWI (CHAC) |
| 10 | Eng.Samson Mloge | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 11 | Ndg.Fredrick Sigachuma | Kny Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi |
| 12 | Ndg.Onolasco Mwogofi | Kny Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 13 | Ndg.Mathias Lyaboga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 14 | Ndg.Mulokozi Kishenyi | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 15 | Ndg.Joyce Mdemwa | Mratibu wa TASAF |
| 16 | Ndg.Keneth A. Mgina | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 17 | Ndg.Demetrio Mgeni | Mthibiti wa Ubora wa Shule |
| 18 | Ndg.Bujah Cosmas | Afisa Ardhi |
| 19 | Ndg.Godfrey Benegula | Kny Afisa Ushirika |
| 20 | Ndg.Boniface Msemwa | Kny Mkuu wa Idara ya Afya |
| 21 | Ndg. Telesphory Myamba | Afisa Biashara |
| 22 | Ndg. Ismail Lugemalila | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi |

MAAFISA TARAFA WALIOHUDHURIA

| NA | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg.Hamza I. Zacharia | Afisa Tarafa – Tarafa ya Imalinyi |
| 2 | Ndg.Emanuel Kingu | Afisa Tarafa – Tarafa ya Mdandu |
| 3 | Ndg.Damas Kavindi | Afisa Tarafa – Tarafa ya Wanging'ombe |

SEKRETARIETI

| NA | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg.Huruma O. Panja | Mwandishi wa Vikao |
| 2 | Ndg.Peter E. Chaula | Mwandishi wa Vikao |

AJENDA ZA KIKAO

1. Kufungua kikao.
2. Kupokea ajenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha kawaida cha Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi na Maliasili cha tarehe 14.04.2021.
4. Kusoma na kujadili utekelezaji wa maazimio ya kikao cha kawaida cha Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi na Maliasili cha tarehe 14.04.2021.
5. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021 kutoka Idara na Vitengo vifuatavyo;
   i. Usafi na Mazingira,
   ii. Ardhi na Maliasili,
   iii. Maendeleo ya Jamii,
   iv. Ujenzi
   v. Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika,
   vi. Mifugo na Uvuvi
   vii. Biashara.
   viii. Ufugaji Nyuki,
6. Mrejesho wa bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021.
7. Kufunga kikao.

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kikao cha tarehe **24.07.2021**, wajumbe wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi, Maliasili na Mazingira walipitisha taarifa za robo ya pili kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 kutoka idara/vitengo vifuatavyo:-

1. Usafi na Mazingira,
2. Ardhi na Maliasili,
3. Maendeleo ya Jamii,
4. Ujenzi,
5. Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika,
6. Mifugo na Uvuvi,
7. Biashara,
8. Ufugaji Nyuki,
9. Mrejesho wa bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021.

MAAZIMIO YA KIKAO CHA KAMATI YA HUDUMA ZA UCHUMI KILICHOFANYIKA TAREHE 24.07.2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI

| NA | AZIMIO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | **MUHTASARI NA.WDC/KHU/04/07/2021/2022**<br>Dondoo Na. 4:3:1:5<br><br>**AZIMIO:**Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri waende kufuatilia fedha/mali za iliyokuwa NJODECO kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe, kikao kijacho taarifa iwasilishwe. | Azimio limezingatiwa, taarifa itawasilishwa kwenye kikao. |
| 2 | **MUHTASARI NA.WDC/KHU/05/07/2021/2022**<br>Dondoo Na.5:2:8:3 | Azimio limezingatiwa, angalia **kiambatisho "A"** |

| | | |
|---|---|---|
| | **AZIMIO:**Kikao kijacho cha Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi, Maliasili na Mazingira iwasilishwe taarifa ya hali/mwenendo wa migogoro ya Halmashauri na Makete, Mfindi na Makambako kuhusu Dampo la Itengelo. | |
| 3 | **MUHTASARI NA.WDC/KHU/05/07/2021/2022**<br>Dondoo Na. 5:6:6:5<br><br>**AZIMIO:**Kikao kijacho iwasilishwe taarifa ya nini kifanyike juu ya namna ya kuwasaidia wafugaji wanaonyanyasika na mradi wa Caritus (kopa ng'ombe lipa ng'ombe). | Azimio limezingatiwa,<br>- Idara ilimwandikia Mkurugenzi wa CARITAS kuja kujadili namna ya kupunguza kero za Wafugaji ambapo ilimuelekeza kuzingatia yafuatayo:-<br>i. Wafugaji waliomaliza Mkataba wasinyang'anywe Ng'ombe na kama ikitokea dosari ya kiufugaji Serikali za Vijiji, Kata na Wataalam husika washirikishwe ili kutafuta ufumbuzi.<br>ii. Wafugaji waruhusiwe kuuza maziwa wanakotaka.<br>iii.Shughuli za matibabu zifanywe na Wataalam wa Serikali tuu ili kuondoa dhana ya bei kubwa wanazotozwa.<br>iv.Sherehe za Wafugaji zinazofanywa kila mwaka zifanyike mara moja kila baada ya miaka miwili ili kuwapunguzia gharama Wafugaji. |
| 4 | **MUHTASARI NA.WDC/KHU/05/07/2021/2022**<br>Dondoo Na.5:2:7:4<br><br>**AZIMIO:**Kikao kijacho iwasilishwe taarifa ya namna ya kutatua suala la maeneo yanayotakiwa kulipwa fidia ambayo Halmashauri ilitenga kwa ajili kujenga Taasisi na wawekezaji kuja kuwekeza. Pia ianishwe orodha ya watu wanaotakiwa kulipwa fidia katika maeneo hayo ya Taasisi na kiasi cha fedha wanachotakiwa kulipwa. | Azimio limezingatiwa, angalia **kiambatisho "B"**. |

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, ninaomba kuwasilisha.

............................

Fredrick E. Mwalongo

**Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi, Ardhi, Maliasili na Mazingira**

C) KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII (ELIMU, AFYA NA MAJI)

I Kikao cha kawaida cha tarehe 24.07.2021

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| NA | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Anaupendo E. Gombela | Diwani Kata ya Mdandu – **Mwenyekiti** |
| 2 | Ndg. Ferd Y. Mhanze | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji - **Katibu** |
| 3 | Mhe. Agnetha J. Mpangile | Diwani Kata ya Ulembwe – Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe - **Mjumbe** |
| 4 | Mhe. Vumilia E. kilamlya | Diwani Viti maalum Tarafa ya Mdandu – **Mjumbe** |
| 5 | Mhe. Silvester J. Kigola | Diwani Kata ya Kijombe - **Mjumbe** |
| 6 | Mhe. Yustin Lunanilo Gudaga | Diwani Kata ya Usuka – **Mjumbe** |
| 7 | Mhe. Oliver H. Myale | Diwani Kata ya Ilembula - **Mjumbe** |
| 8 | Mhe. Jelitha A. Fute | Diwani Viti maalum Tarafa ya Wanging'ombe – **Mjumbe** |
| 9 | Mhe. Essau Th. Sanga | Diwani Kata ya Malangali – **Mjumbe** |
| 10 | Mhe.Thobias M. Mkane | Diwani Kata ya Itulahumba - **Mjumbe** |
| 11 | Mhe. Wiston E. Mbilinyi | Diwani Kata ya Kidugala – **Mjumbe** |
| 12 | Mhe. Mussa A. Sanga | Diwani Kata ya Kipengere - **Mjumbe** |
| 13 | Mhe. Halfan R. Kawambwa | Diwani Kata ya Uhenga - **Mjumbe** |

WAKUU WA IDARA/VITENGO WALIOHUDHURIA

| NA | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Odetha Banige | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |
| 2 | Ndg. Amon P. Chalamila | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 3 | Ndg. Severine M. Mfuse | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki |
| 4 | Ndg. Frank Ngogo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira |
| 5 | Ndg. Frederick Sigachuma | Kny Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi |
| 6 | Ndg. Telephory Myamba | Afisa Biashara |
| 7 | Ndg. Albert Mwakipesile | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 8 | Ndg. Rukia Mwelelwa | Katibu TSC |
| 9 | Ndg. Onolasco Mwogofi | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 10 | Ndg. Carystus E. Kihaka | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 11 | Ndg. Vista Chapile | Kny Mratibu wa Mapambano Dhidi ya UKIMWI (CHAC) |
| 12 | Ndg. Godfrey Benegura | Kny Afisa Ushirika |
| 13 | Ndg. Mohamed Ilunga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 14 | Ndg. Yusufu Yahaya | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 15 | Ndg. Ismail M. Lugemalila | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 16 | Ndg. Demetrio K. Mgeni | Mthibiti Ubora wa Shule |
| 17 | Ndg. Witness Mfikwa | Kny Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 18 | Ndg. Bujah Cosmas | Afisa Ardhi |
| 19 | Mhandisi Samson Mloge | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 20 | Ndg. Joyce Mdemwa | Mratibu wa TASAF |
| 21 | Dkt. Frank Chiduo | Mkuu wa Idara ya Afya |

MAAFISA TARAFA WALIOHUDHURIA

| NA | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Hamza I. Zacharia | Afisa Tarafa – Tarafa ya Imalinyi |
| 2 | Ndg. Emanuel J. Kingu | Afisa Tarafa – Tarafa ya Mdandu |
| 3 | Ndg. Damas Kavindi | Afisa Tarafa – Tarafa ya Wanging'ombe |

SEKRETARIETI

| NA | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Ndg. Peter E. Chaula | Mwandishi wa Vikao |
| 2 | Ndg. Huruma O. Panja | Mwandishi wa Vikao |

AJENDA ZA KIKAO

1. Kufungua kikao.
2. Kupokea ajenda za kikao.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha kawaida cha Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji) cha tarehe 15.04.2021.
4. Kusoma na kujadili utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha kawaida cha Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji) cha tarehe 15.04.2021.
5. Taarifa za utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021, kutoka Idara na Vitengo vifuatavyo:-
    i. Afya,
    ii. Elimu Msingi,
    iii. Elimu Sekondari,
    iv. TSC na
    v. Mthibiti Ubora wa Shule.
6. Mrejesho wa Bajeti ya Halmashauri kwa shughuli za maendeleo na matumizi ya kawaida kwa mwaka 2021/2022.
7. Taarifa ya Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na mapendekezo.
8. Taarifa ya Rasimu ya Sheria Ndogo ya Uanzishaji wa Mfuko wa Elimu 2021 katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.
9. Mapendekezo ya usimamizi na uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (i-CHF).
10. Mapendekezo ya gharama za uchangiaji kwenye vituo vya huduma za afya kuanzia Julai Mosi 2021.
11. Kufunga kikao.

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kikao cha tarehe **24.07.2021**, wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji) walipitisha taarifa za idara/vitengo vifuatavyo;

i. Afya,
ii. Elimu Msingi,
iii. Elimu Sekondari,
iv. TSC na
v. Mthibiti Ubora wa Shule.

Vile vile walipitisha taarifa na mapendekezo yafuatayo:-

1. Taarifa ya Mrejesho wa Bajeti ya Halmashauri kwa shughuli za maendeleo na matumizi ya kawaida kwa mwaka 2021/2022.
2. Taarifa ya Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na mapendekezo.
3. Taarifa ya Rasimu ya Sheria Ndogo ya Uanzishaji wa Mfuko wa Elimu 2021 katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.
4. Mapendekezo ya usimamizi na uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (i- CHF).
5. Mapendekezo ya gharama za uchangiaji kwenye vituo vya huduma za afya kuanzia Julai Mosi 2021.

**UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII (ELIMU, AFYA NA MAJI) KILICHOFANYIKA TAREHE 24.07.2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI**

| NA | AZIMIO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | Muhtasari Na. WDC/KHJ/4/07/2021/2022<br>Dondoo Na. 4:3:7:1<br><br>Ifikapo mwezi Oktoba, 2021 jitihada ziaze kufanyika za usajili wa shule mpya za sekondari zinazojengwa kwenye Kata za Uhenga, Kidugala, Malangali na Shule Maalum ya Wavulana ya Sekondari Isatu. | Mchakato wa usajili bado haujaanza inasubiriwa ujenzi wa majengo yanayohitajika ukamilike ndiposa uanze mchakato wa usajili. |
| 2 | Muhtasari Na. WDC/KHJ/4/07/2021/2022<br>Dondoo Na. 4:3:7:1<br><br>Taarifa ya ujenzi wa shule mpya za sekondari katika Kata za Malangali, Kidugala na Uhenga iwe inawasilishwa kwenye kila kikao cha Kamati ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji). | Taarifa imeandaliwa, angalia Kiambatisho "**A**". |

***Mheshimiwa Mwenyekiti***, ninaomba kuwasilisha.

…………………………

Anaupendo E. Gombela

**Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Jamii**

**(Elimu, Afya na Maji)**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MKOA WA NJOMBE

# HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI – SEPTEMBA (ROBO YA KWANZA) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22


**Imetayarishwa na;**

**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,**
**Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe,**
**S.L.P 64,**
**WANGING'OMBE – TANZANIA**


***Oktoba, 2021***

**MUHTASARI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI – SEPTEMBA (ROBO YA KWANZA) KWA MWAKA 2021/22**

Mhe. Mwenyekiti
Baraza la Madiwani,
**Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe**

Katika Mwaka wa fedha 2021/22 kiasi cha Tshs. 9,982,566,000.00 kiliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Kiasi hicho kinajumuisha Shs. 4,818,666,000.00 fedha za ndani na Shs 5,163,900,000.00 fedha za nje. Kiasi cha Shs. 1,207,000,000 kiliidhinishwa ikiwa ni fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuchangia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2021, jumla ya Shs. 741,572,513.6 zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Maendeleo ikiwa ni sawa na 7.39% ya fedha iliyokisiwa. Fedha zilizopokelewa zinajumuisha Idara za Afya na Elimu

Fedha hizi zinaendelea kutekeleza Miradi ya Maendeleo katika maeneo mbalimbali katika Halmashauri yetu kwa Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

Katika taarifa hii, kuna utekelezaji wa Miradi Viporo kwa Mwaka 2020/2021 ambayo imeendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/2022. Miradi hiyo inapatikana katika majedwali Ukurasa wa **01 - 03**

Kwa ujumla hali ya utekelezaji wa Miradi katika Robo hii ya kwanza ya mwaka 2021/22 umekuwa wakusuasua kwa kuwa miradi mingi ya maendeleo bado haijapokea fedha kutoka Serikali Kuu. Aidha, Utekelezaji wa shughuli za Maendeleo katika kipindi cha Robo hii umekuwa na changamoto nyingi kwa kuwa Serikali Kuu (Wizara ya Fedha na Mipango) haijaleta fedha kwa ajili ya kumalizia na kuanza Ujenzi wa Miradi Mikubwa na Midogo ndani ya Halmashauri. Michanganuo hiyo inapatikana ukarasa wa **04 -17**

Aidha, Halmashauri imepokea fedha kiasi cha Shs.456,694,231.00 ikiwa ni ongezeko la bajeti ya Mwaka 2021/2022 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Idara za Elimu na Afya. Michanganuo hiyo ipo katika ukuarasa wa **18 -19**

Muhtasari huu umeambatana na majedwali ya ufafanuzi wa utekelezaji katika shughuli za maendeleo kwa kila Sekta na vyanzo vya fedha pamoja na hali halisi ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Naomba kuwasilisha,

Maryam A. Muhaji
Mkurugenzi Mtendaji (W)
**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (BAKAA MWAKA 2020/21)

1. IDARA YA AFYA - FEDHA ZA SERIKARI KUU

| NA | MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA | KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA | CHANZO CHA FEDHA | ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI | KIASI CHA FEDHA KILICHOTENGWA | KIASI CHA FEDHA KILICHOTUMIKA | SALIO (BAKAA) | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa kituo cha Afya Saja kata ya Saja | 500,000,000 | Serikari kuu | Kata ya Saja | 500,000,000.00 | 86,519,800.00 | 413,480,200 | Utekelezaji unaendelea Jengo la Kuhifadhia maiti lipo hatua ya kumimina renta na Nyumba ya mtumishi pamoja na chumba cha upasuaji vipo hatua ya kuinua kuta na jengo la maabara na Mama na Mtoto vipo hatua ya umiminaji wa jamvi. |
| 2 | Ujenzi wa kituo cha Afya Ilembula Kata Ilembula | 500,000,000 | Serikari kuu | Kata ya Ilembula | 500,000,000.00 | - | 500,000,000 | Nguvu za Wananchi zinaendelea kutumika kazi na utaratibu wa kuanza kutumia fedha tajwa unaendelea pia. |
| | **Jumla** | **1,000,000,000** | | | **1,000,000,000.00** | **86,519,800.00** | **913,480,200** | |

2. IDARA YA ELIMU SEKONDARI - FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO

| NA | MRADI/SHUGHULI ILIYOPANGWA | KIASI CHA FEDHA KILICHOIDHINISHWA | CHANZO CHA FEDHA | ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI/SHUGULI | KIASI CHA FEDHA KILICHOTENGWA | KIASI CHA FEDHA KILICHOTUMIKA | SALIO (BAKAA) | HALI HALISI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Madarasa Matatu (3) Sekondari ya Kidugala | 60,000,000 | Serikali Kuu | Kidugala Sekondari | 60,000,000 | 26,384,400.00 | 33,615,600 | Ujenzi unaendea |
| 2 | Ujenzi wa matundu kumi (10) ya Vyoo Kidugala Sekondari | 11,000,000 | Serikali Kuu | Kidugala Sekondari | 11,000,000 | 4,321,000.00 | 6,679,000 | Ujenzi unaendelea |
| 3 | Ujenzi wa nyumba ya Mwalimu (2 in 1) Shule ya Sekondari Kidugala | 50,000,000 | Serikali Kuu | Kidugala Sekondari | 50,000,000 | - | 50,000,000 | Utekelezaji utaanza kota ya Pili. |
| 4 | Ujenzi wa Madarasa Matatu (3) Sekondari ya Malangali | 60,000,000 | Serikali Kuu | Malangali Sekondari | 60,000,000 | 10,519,000.00 | 49,481,000 | Ujenzi unaendelea |
| 5 | Ujenzi wa matundu Kumi (10) ya Vyoo Malangali Sekondari | 11,000,000 | Serikali Kuu | Malangali Sekondari | 11,000,000 | - | 11,000,000 | Utekelezaji utaanza robo ya Pili |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Ujenzi wa nyumba ya Mwalimu (2 in 1) Malangali Sekondari | 50,000,000 | Serikali Kuu | Malangali Sekondari | 50,000,000 | 2,850,000.00 | 47,150,000 | Ujenzi unaendelea |
